# *Kutoka Kwa Tatu*

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui kama kuna maombi yoyote maalum ungetaka yajulikane mbele za Mungu. Inua tu mkono wako na, chini tu ya mkono wako, shikilia tu ombi lako.

2 Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya jambo hili, wakati mwingine wa kukusanyika pamoja, upande huu wa Umilele. Na tunatarajia asubuhi ya leo kuhuishwa upya kwa nguvu kuja kutoka Kwako, zipate kututia moyo kwa ajili ya safari iliyoko mbele. Tumekusanyika kama wana wa Kiebrania walivyofanya asubuhi na mapema, kuokota mana iliyokuwa imetolewa kwa ajili yao usiku kucha, kuwapa nguvu kwa ajili ya siku ijayo. Tunakusanyika kwa ajili ya Mana ya kiroho, asubuhi ya leo, ipate kutupa nguvu kwa ajili ya safari.

3 Chini ya kila mmoja wa mikono hiyo iliyoinuliwa, Wewe unajua yote wanayohitaji, Bwana. Nami ninaomba ombi langu, pamoja na yao, mbele Zako, kwamba utakidhi kila haja waliyo nayo. Waponye wagonjwa na wanaoteseka, Bwana. Tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu, na unaweza kufanya mambo yote, na umeahidi kuyafanya kama tungefanya tu kama vile wimbo ulivyotushauri, *Amini Tu*, na kama vile tulivyoyasikia maneno haya mazuri sana, *Tembea na Uzungumze Na Mfalme*.

4 Sasa, Baba, Mungu, libariki Neno Lako linapohubiriwa asubuhi ya leo, na jalia lipate mahali Pake pa kutulia mioyoni mwetu, lipate kuleta mambo tuombayo, Baba. Katika Jina la Bwana Yesu tunaomba hayo. Amina.

Mwaweza kuketi. Asante, dada.

5 Ninaamini imekwisha kusemwa, "Nilifurahi waliponiambia, 'Na twende nyumbani kwa Bwana.'"

6 Tulipokuwa tukiondoka Hot Springs, jana, Ndugu Moore alikuwa akisema, "Ndugu Branham," kasema, "wewe, hivi huwezi kwenda kwa gari pamoja nami huko chini, Texas, kwenye mkutano kule chini," kasema, "upumzike siku kadhaa?"

7 Nikasema, "Nina ibada mbili kesho."

Akasema, "Ati ibada mbili?"

Nikasema, "Naam."

8 Kasema, "Unavyohubiri hapa kwa nguvu," kasema, "mtu anapaswa kupumzika juma moja baada ya kila moja ya hayo." Kasema, "Hebu mchukue mchungaji, anatoa ujumbe wake wa Jumapili asubuhi, na kadhalika," kasema, "kisha anapumzika juma zima. Na, halafu, na labda huo utakuwa ni wa dakika

thelathini, ama kitu kama hicho." Kisha kasema, "Ulihubiri kama saa mbili ama tatu hapa, wakati mmoja," kasema, "halafu, siku baada ya siku, na wakati mwingine mara mbili kwa siku, kisha unafanyiza mstari wa maombi, utambuzi huo wote." Kasema, "Sasa unasema unaenda nyumbani, uwe na ibada mbili Jumapili?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Kasema, "Unafanyaje jambo hilo?"

Nikasema, "Msaada wangu hutoka kwa Bwana." Unaona?

9 Wakati umeenda sana, kama vile mmoja, mtu fulani alivyosema muda mfupi uliopita, katika maombi, wakati tu nikiingia. Wakati umeenda sana, na uhitaji ni mkubwa, na sisi tuko hapa kujaribu kuchangia sehemu yetu, kuusaidia wakati huu mkuu tulimo ndani yake.

10 Sasa, Bwana akipenda, usiku wa leo, ninataka kuzungumza juu ya somo, "Je! maisha yako yanaistahili Injili?" Huo, ninataka kuurekodi huo kwenye kanda.

11 Na sasa, sijui kama wataurekodi huu kwenye kanda asubuhi ya leo, ama la. Ninaona baadhi kwenye kile chumba. Kuna—kuna baadhi ya jamaa hao mle ndani; nadhani wanaurekodi. Nilininii. . . Nilidhani Ndugu Neville angefanya jambo hili. Nilimwomba, Jumapili iliyopita, kwamba tu awe na ninii yake. . . aendelee na ujumbe wake; kisha aendelee, aniruhusu niingize tu jambo fulani nyuma yake. Lakini, endapo wanataka kulirekodi kwenye kanda somo hili la shule ya Jumapili, mbona, itakuwa ni sawa.

12 Na halafu, Bwana akipenda, Jumapili ijayo, hiyo ni kusema, Bwana akituruhusu na tukiwa hapa, ninataka kuzungumza juu ya somo ambalo nimekuwa nikitaka kuzungumzia kwa muda mrefu, na nikaahidi ningehubiri Jumbe kama hizo kutoka maskanini, kwanza, hizo Jumbe zilizorekodiwa. Ninataka kukishtaki kizazi hiki kwa kumsulibisha Yesu Kristo; Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda.

13 Na sasa, usiku wa leo, kwenye saa moja, ama saa moja na nusu, ni ninii—ni ujumbe wa "Je! maisha yako yanastahili?"

14 Sasa, wakati mwingine, katika kuzungumza juu ya Jumbe hizi namna hiyo, ninasema mambo ambayo ni makali sana. Nami kweli siyakusudii kwa kanisa hili hapa, ama chochote kile. Kumbukeni, wakati nikihubiri, huo unazunguka ulimwenguni kote. Unaona? Nasi tuna huduma ya kanda, kote ulimwenguni, nao wanazipeleka Jumbe hizi huko misituni na kila mahali. Na Roho Mtakatifu wakati mwingine ananiongoza kusema jambo fulani ambalo huenda likawa ndilo jambo ambalo ndilo hasa analolitaka kwa ajili ya mtu fulani huko mbali Austaralia, mahali fulani, ama chochote kile. Kwa hiyo, labda, hali fulani, ungesema, "Vema, sasa, hali hiyo haipo hapa. Kwa nini anasema

jambo hilo?" Labda ni kwa ajili ya mahali pengine, unaona. Kwa hiyo, naam, nina hakika ninyi watu mnalielewa jambo hilo, ya kwamba Jumbe hizi hazielekezewi yeyote. Zinaelekezwa tu kwa Kanisa, kwa jumla, kila mahali, na chochote Bwana angetuongoza kusema na kutenda.

15 Nilikuwa na wakati mzuri sana huko Hot Springs, na kwenye mkutano wa mtindo wa kale wa Kipentekoste. Nina hakika wengi wenu mmeridhika ambao ni Wapentekoste kule chini, tangu ninyi—ninyi mlipokwenda kule. Vema, ninii tu, silijui kundi hilo. Nilipaswa tu kushuka kwenda kule kwa juma moja, nami nikatoa siku mbili ama tatu. Lakini ninataka kusema jambo moja. Katika mkutano huo, hakika walikuwa na imani, kuamini. Kama yeyote wenu alikuwa kule . . .

16 Ambalo, ninajua, mama huyu hapa, anayeketi pembeni, sijui yeye ni nani. Ama, papa hapa, ninajua yeye alikuwa kule. Na ninajua ndugu kadhaa waliokuwa kule, Ndugu Jackson, hao, Ndugu Palmer.

17 Hayo ndiyo watu wanayopata wakiwa na imani. Mnaona? Mnaona mstari huo wa maombi? Hapakuwapo na mtu aliyeingia ama aliyetoka pasipo kuponywa na Mungu. Unaona? Unaona? Na kwa hiyo, unapokuwa na imani . . .

18 Na jambo lingine, huenda ikawa kuna baadhi yenu, huenda msielewe na mhemuko huo, kucheza, kupaza sauti. Vema, wao wananinii tu . . . Hawamwangalii mtu yeyote maalum. Wanapaza tu sauti, mbele za Mungu. Unaona? Hilo ni sawa.

19 Lakini, ninataka kusema, ndilo moja ya—moja ya makundi safi sana ya wanawake niliyopata kuona, hizo nywele ndefu, na—na watu wanaotoka huko nyuma msituni, huko nyuma vichakani. Ila siamini nilimwona mtu yeyote ambaye kwa namna fulani anaonekana wa kisasa, mnajua ninalomaanisha, akiwa amejipaka kila namna ya vipodozi na kadhalika. Inaonyesha. Huenda nisikubaliane nao katika yote wanayofundisha, bali hakika ninaweza kukubaliana nao hapo. Hao walionekana kama ni Wakristo, kwangu mimi.

20 Kwa hiyo Bwana aliniongoza kuzungumza juu ya somo, jana, ama juzi, adhuhuri: *Mara Nyingine Tena Tu, Bwana*. Na huko kanisani, baadhi yao kule hawakujua, nilifanya jambo hilo kwa makusudi fulani, kwa maana Bwana aliniongoza kufanya hivyo. Maskini kundi hilo lilikuwa likichukuliwa kwenye jambo fulani, na Bwana akanisaidia kwa hilo ku—kufanya jambo hilo. Kwa hiyo, lilikuwa ni zuri sana. Hakika mimi . . .

21 Unajua, mambo huendelea, kama huna jicho la kiroho, hulipati. Unaona? Inakubidi kuyatarajia mambo hayo.

22 Niliingia. Na huyu Ndugu Ungren, hiyo ni kama mara ya pili nimewahi kumsikia mtu huyo akiimba. Mara nilipokuwa nikiingia hicho chumba, yeye alikuwa akiimba *Ninatembea na Kuzungumza Na Mfalme*. Nikawaza, "Huo si ni mzuri

sana!" Jinsi ambavyo Mfalme alipata . . . Unaona? Kutembea na kuzungumza, hiyo inamaanisha ni ushirika mfululizo sikuzote. Sio kanisani tu, bali, kila mahali, kutembea na kuzungumza na Mfalme.

23 Na hapo, nikaangalia juu kwenye ukuta, na kulikuwako na kadi iliyokuwa imechomoza kwenye picha ndogo mle ndani, ya namna fulani ya mandhari ambayo mtu anayeitwa George Todd ali—alikuwa amenichorea. Sijui ni kwa nini mtu huyo alifanya hivyo. Labda, huenda ikawa, kamwe hakuwazia, naye alikuwa ameichora na ni picha ya mlima, mbali huko msituni, na—na kijito kikibubujika kama viwimbi. Na upande wa pili wa kijito hicho, amesimama mama kulungu na mtoto wake, wameinua maskio yao, wakiangalia ng'ambo ya pili ya kijito hicho. Sijui kama Bw. Todd yupo hapa. Simjui. Lakini, ninataka kusema jambo hili, Bwana alinena nami wakati nilipoitazama picha hiyo. Na labda yeye hakujua, wakati alipokuwa akiichora.

24 Mnakumbuka hadithi yangu ndogo kuhusu yule kulungu ambaye yule jamaa alikuwa akitaka kumpiga risasi, na kuita kwake? Vema, yeye yuko huko na mtoto wake, kwa hiyo, karibu na maji ya uzima. Unaona? Uvuvio, jinsi ambavyo mama kulungu huyo na mtoto wake walikuwa pale! Nami nikawaza, "Naam. Na upande wa pili, ambapo pana, karibu na miti ya kijani kibichi daima, mimi nina ma—mama na mtoto kule, pia, wanaongojea kule."

25 Asante, ndugu, Ndugu George Todd, iwapo mtu huyo yupo hapa asubuhi ya leo.

26 Sasa, ningefanya somo la shule ya Jumapili. Kwa kawaida mimi huchukua muda mrefu nalo.

27 Kuna kitu kinachochezacheza wakati wote moyoni mwangu, sijui, tangu jana. Sasa sisi . . . kama Bwana . . . ni—ni somo. Mimi ninazeeka, wala si—sijui nitakuwa hapa muda gani zaidi. Lakini kuna swali kubwa kanisani, ambalo limewafanya watu wahitilafiane, na mawazo mbalimbali.

28 Ni kama kule kula kwa "lile tofaa." Nami nilihubiri juu ya Ujumbe huo, na ninaamini, kwa dhati, ninaweza kulithibitisha kwa Maandiko, ya kwamba halikuwa ni matofaa. Unaona? Lilisababisha kuchanganyikiwa kwingi sana.

29 Kwa hiyo, labda, kabla hatujaondoka . . . Inatupasa kurudi sasa, katika muda wa siku thelathini hivi, unajua, kurudi Arizona. Na kwa hiyo kama, kabla sijaondoka, Bwana akipenda, ningependa kuchukua Maandiko. Na msiurekodi. Kama wakiurekodi, msiiuze kanda hiyo. Msiisambaze. Ninataka kuelezea ukweli halisi wa ndoa na talaka. Ni swali. Na hizi ndizo saa za mwisho, ambapo, "Wakati siri zote za Mungu zinapaswa kumalizika." Na jana, nikiivuka milima, karibu na macheo, Roho Mtakatifu alionekana kuwa ananiambia, "Rekodi

huo kwenye kanda na uuweke akiba," sijui ni kwa nini, lakini, "Ukweli halisi wa ndoa na talaka."

30 Baadhi yao husema, "Watu wanaweza kuoa, kama wanaweza kuapa walikuwa katika uzinzi." Na wengine husema, "Vema, kama wakitesana, na—na hawawezi kuishi pamoja; ni afadhali kuishi, duniani, kwa amani, kuliko kuishi katika kuzimu duniani." Na maswali hayo yote mbalimbali! Na wengine wanawaoza kwa njia yoyote ya zamani. Na wengine wanataka kuwanyunyizia maji matakatifu, na kuwarudisha, na kusema, "Kabisa wao hawajawahi kufunga ndoa." Na wakawabariki, na kuwarudisha kanisani tena. Kuna kila namna ya vurugu. Lakini, kama kuna vurugu kiasi hicho, kuna Ukweli mahali fulani.

31 Ninaamini, na ninasema hili kwa uchaji, ninaamini Bwana amenifunulia huo, na mimi . . . Ukweli. Na kama ungeingia miongoni mwa makanisa, ungekirarua kitu hicho vipande-vipande. Ambalo, labda unapaswa kufanya. Lakini ni ninii . . . Afadhali niwaachie tu wachungaji, niwaachie tu wachungaji wa makanisa, wachukue kanda hiyo. Na hebu na waicheze, na ndipo wanaweza kuongoza kutoka hapo na kuendelea. Lakini ningetaka tu kuunasa huo, kuonyesha Ukweli wake halisi. Ninaamini huu ndio wakati ambapo hizi "siri zitamalizika," zitakamilishwa. Zimefikiwa, kama tulivyosema, kote katika nyakati, za kanda, kama tulivyoielezea ile *Mihuri Saba*, na *Nyakati Saba za Kanisa*.

32 Na sasa tunaelekea wakati wa zile *Baragumu Saba*, na halafu vile *Vitasa*. Na labda tungeweza kupanga mkutano wa majuma mawili na kuziweka zote mbili pamoja. Ningetaka zirekodiwe kwenye kanda.

33 Na halafu, mbali na hayo, ninajaribu sasa kisahihishwe prufu, na kuchapisha vitabu kutoka kwa hicho, vya *Nyakati za Kanisa*; vitabu saba vya wakati wa kanisa, kanda saba, na kuvifanya namna hiyo. Tunaweza kufanya kazi hiyo kwa bei nafuu tuwezavyo, kusudi kila mtu aweze kukipata. Halafu, Bwana akikawia, nami niondoke, mtaona ya kwamba mambo niliyosema katika Jina la Bwana yatatimia jinsi tu yalivyosemwa. Hayajashindwa kamwe, bado, na baadhi yao hayana budi kutimia baadaye.

34 Na mimi—mimi natumaini ya kwamba Bwana ametuwezesha kufanya jambo hilo mara moja. Tutawatangazia watu, wakati fulani, kwa maana kuna wengi wanaotaka kuja na kuyasikia mambo hayo. Nami—nami ninathamini jambo hilo.

35 Kama hakuna mtu aliyeuamini Huo, ama kuusikiliza, ingenifaa nini, kusimama hapa, kusema lolote juu Yake? Unaona? Ingekuwa ni kama kutupa mkate majini. Ingekuwa ni kama . . . Kama hakuna mtu angaliuamini, basi ingekuwa ni kama kuwatupia nguruwe lulu. Bali kuna maelfu mara maelfu wanaouamini Huo. Unaona? Na wanashikilia kila Neno. Na

tungetaka kuwaingiza wengi, iwezekanavyo, wakati tutaninii—tutakapokuwa tayari kufanya ibada hizi, na kwa utukufu wa Bwana. Na tunatumaini ya kwamba Mungu atatupa hilo.

36 Na sitaki kulifanya hilo mpaka nimevuviwa Kiungu kulifanya. Mungu anao wakati kwa kila kitu. Unaona? Haikupasi kuutangulia. Kama ukikata ngano yako kabla... Wakiweka kivuna mle ndani kabla haijaiva, utapoteza sehemu kubwa ya ngano yako. Unaona? Kwa hiyo, wakati mundu ukiwa tayari kuingizwa, Mungu atauingiza kazini, ndipo tutaanza kuvuna. Lakini ninanii tu...

37 Wakati, ninajisikia kusukumwa namna hiyo. Nilidhani ningejitikisa nitoke katika hilo, katika muda mfupi. Siku nzima jana, nisingeweza kuliondoa moyoni mwangu, usiku kucha jana usiku. Nililala karibu saa sita. Nilipata karibu saa tatu za usingizi, usiku wa juzi. Na jana usiku nisingeweza kulala. Bado, Kitu Fulani kilisema, "Rekodi huo, *Ndoa Na Talaka*." Unaona? Kwa hiyo mimi—mimi... Bwana akipenda, kama hilo likidumu moyoni mwangu na Bwana anifunulie mengi zaidi kulihusu, vema, basi, nitaninii... Hu—huenda nikaurekodi huo. Unaona?

38 Lakini, kumbukeni, ni kwa ajili ya wahudumu tu. Ninyi njoni, ila, na msikilize. Lakini kanda yenyewe, hebu... Unaona, maana ikiingia miongoni mwa makusanyiko, na wengine wako *hivi*, na wengine *vile*, na kutoa maoni yao wenyewe. Nami ninawataka ndugu wahudumu wawe na huu kwenye chumba chao cha kusomea, na kisha waanzie hapo, maana hao ndio wanaowajibika. Hao ndio wanaowajibika. Kama kushuka kwenda kumchezea hakimu, baadhi ya hawa mamwinyi. Naam.

39 Tuone yale Bwana aliyosema juu ya huu, *Ndoa Na Talaka*. Ni mtakatifu kuliko vile watu wanadhani ulivyo. Nao utashikamana moja kwa moja na *Uzao wa Nyoka*. Ni jambo lile lile, likiendelea moja kwa moja, hizo ndizo zile siri. Kumbukeni, "Katika siku za malaika wa saba, siri zote za Mungu zinapaswa kutimizwa," yale mambo yasiyojulikana ambayo Bwana atayatimiza. Sasa, umbali huu...

40 Sasa kumbukeni, mnaanza mkutano wenu saa moja na nusu. [Ndugu Neville anasema, "Naam."—Mh.] Sasa, Ndugu Neville, kama una ujumbe kwa ajili ya usiku wa leo, uhubiri. Unaona? ["La, bwana."] Haitanichukua kama saa moja ama dakika arobaini na tano, nami nitaurekodi huo mwingine.

41 Ninapenda kumsikiliza Ndugu Neville. Ninampenda. Yeye ni ndugu yangu. Na mimi na—nafikiri yeye ni mhubiri mzuri sana, mhudumu wa ajabu sana. Na mimi... Jambo moja kuhusu Ndugu Neville, ninalolipenda, anaposema jambo lolote, yeye huyaishi yale anayonena habari zake. Sasa, hilo—hilo ndilo jambo muhimu.

42 Unajua, unaweza kumwishia mtu mahubiri kuliko unavyoweza kumhubiria mamoja. "Kwa maana ninyi wenyewe

ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote. Sasa, hebu, kabla hatujaninii . . .

43 Tunaweza kufungua kurasa, bali Mungu hana budi kulifungua somo hili la shule ya Jumapili, kwa hiyo hebu na tumwombe tu afanye jambo hilo.

44 Baba wa Mbinguni, sisi—sisi kwa imani tunaangalia kwenye mambo ya usoni. Ninaangalia sasa, kwa imani, kwenye jambo fulani lijalo, Bwana, juu ya nchi, ambalo litawavuta watu Wako pamoja. Tunapoyaona makanisa ya kimadhehebu yakikaza sana na kuwa tofauti sana, kweli yanawasukumia watu nje; kama tu ilivyokuwa huko Misri, farao akiinuka, asiyemjua Yusufu.

45 Kama ilivyokuwa huko Ujerumani, na—na hadi huko juu Urusi, na Italia, watu waliwainua akina Yusufu, Hitler na Stalin, Mussolini, ambao waliwachukia Wayahudi. Iliwalazimu kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Mungu, Wewe una njia za kufanya mambo, ambazo hatuzifahamu. Na uliwashurutisha. Hakuna makao Ujerumani; walinyang'anywa kila kitu. Pia, huko Italia, Urusi, hakuna mahali pa kwenda. Nao wakarudishwa kwenye nchi ya uenyeji wao, ili kulitimiza tu Neno.

46 Loo, mkono wa Mungu wenye upendo! Jinsi ambavyo, wakati mwingine, unaonekana ni mkatili, jinsi watu wanavyoteseka, bali huo, bado, ni mkono wa Yehova wenye upendo, ukiwaongoza watoto Wake wadogo. Tunakushukuru, Bwana.

47 Sasa ninaomba, Mungu, ninapoiona siku ambapo dhehebu linawasukuma waaminio, likiwafukuza, likisema, ya kwamba, "Jina lao halina budi kuwa kwenye kitabu chao, vinginevyo wamepotea. Hawana uhusiano wowote na kundi hilo lingine." Ni ule mkono tu wa Yehova wenye upendo, ukiwaongoza kwenye Mti wa Uzima. Ninaomba, Mungu, ya kwamba, kila mmoja. Ninajua watafanya hivyo. Kwa maana, ni Neno Lako, wala haliwezi kushindwa. Na jalia tuongozwe kwenye Mti wa Uzima, ili tuweze kuwa mmiliki wa Uzima wa Milele, kuuona mkono wa Mungu, na, kwa macho ya imani, tuangalie kupita vivuli hivi tunamotembelea leo, tuione ile Nchi ya ahadi ikiwa hapo mbele tu.

48 Libariki Neno Lako, asubuhi ya leo, Bwana, Maandiko haya machache na mihtasari niliyoandika hapa chini. Jalia Roho Mtakatifu aje sasa, ninapojiweka wakfu, kutahiriwa kwa ulimi na wazo, moyo. Na kanisa liyaweke wakfu maskio yao ya ufahamu, mioyo yao, na sisi sote, pamoja, ili Wewe upate kusema nasi kupitia Neno Lako, kwa maana Neno Lako ni Kweli. Katika Jina la Neno, Yesu Kristo, tunaomba hayo. Amina.

49 Sasa, fungueni kwenye Biblia zenu, kwenye Kitabu cha Kutoka. Na sasa ninataka kusoma sehemu ya Maandiko kutoka katika Kutoka, mlango wa 3, kuanzia 1 hadi 12. Sikilizeni tu, kwa makini, tunaposoma. Kutoka, mlango wa 3, 1 hadi 12.

*Basi huyo Musa alikuwa akichunga* makundi *ya Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani; akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu, hata Horebu.*

*Malaika wa* B*WANA* *akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikakati ya kijiti; na* ninii*. . .yeye. . . akatazama, na kumbe! Kile kijiti* kiliwaka *moto, nacho kijiti hakikuteketea.*

*Musa akasema, Nitageuka sasa, niyaone maono haya makubwa,* ambapo *kijiti hiki. . .kijiti hiki hakiteketei.*

B*WANA* *alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame,. . .*

50 Ninataka kutia mkazo kwenye hilo!

B*WANA* *alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema, Musa! Musa! Akasema, Mimi hapa.*

*Naye akasema, Usikaribie hapa;* ila *vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu.*

*Tena akasema, Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.*

B*WANA* *akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri,. . .nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua* maumivu *yao;*

*Nami nimeshuka ili niwaokoe na* mikono *ya* Mmisri, *niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema,. . .na* nchi *pana;* na *nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Wakanaani,. . .Wahiti,. . .Wahivi,. . .Myebusi.*

*Basi, tazama, kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia; tena nimeyaona hayo mateso ambapo Wamisri* wamewatesa.

*Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao,. . .*

51 Unaona? "Nimeshuka." Lakini, "Ninakutuma wewe." Mungu, akienda katika umbo la mwanadamu. "Nenda." Hebu nisome kifungu cha 10 tena.

*Haya, basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri.*

*Musa akamwambia Mungu, Mimi ni nani, hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli watoke Misri?*

*Akasema, Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe; na dalili ya kuwa nimekutuma ndiyo hii;* utakapokuja huku. . . .

52 Samahani.

> . . . *Utakapokuwa umekwisha kuwatoa hao watu katika Misri, mtamwabudu Mungu katika mlima huu.*

53 Bila kuona, hapo kabla, bali nikijisikia kuvuviwa sana na Roho asubuhi ya leo, nilishika jambo hilo papo hapo. Mungu, akimtuma mtumishi Wake arudi mahali alipokuwa amepatoroka, Yeye alimpa ishara ya mlima. Kamwe sikuliona mpaka wakati huo tu. "Hii itakuwa ndiyo dalili ya Milele kwako." Mnaona?

54 Sasa tutazungumza, asubuhi ya leo, juu ya somo la kutoka kwa pili kwa watu wa Mungu, ama kuitwa kwa watu wa Mungu watoke. *Kutoka* maana yake ni "kutolewa; kuitwa watoke; kuondolewa kutoka." Na ninataka kutumia hilo kama somo, la kutoka kwa pili kwa watu wa Mungu. [Ndugu Branham anakuita, *Kutoka Kwa Tatu*, katika ibada ya jioni—Mh.]

55 Sasa, wamekuwa na kutoka kwingi, hakika, bali ninazungumzia wakati ambapo Mungu aliagiza kutoka, kujitenga na mahali walipokuwa, kwenye wakati wa sasa. Hapa, Mungu anajiweka tayari kulitimiza Neno Lake lililoahidiwa Kiungu ambalo alikuwa amempa Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo. Miaka, mamia ya miaka yalikuwa yamepita, lakini, bado, Mungu kamwe haisahau ahadi Yake. Katika majira yake, kwenye wakati unaofaa, Mungu daima hutimiza ahadi Yake.

56 Kwa hiyo, unaweza kuwa na hakika ya kwamba kile Mungu ameahidi katika Biblia hii, Yeye atakitimiza. Hakuna haja kabisa ya kujaribu kuwazia jambo lingine lolote, na kusema, "Vema, nabii alikuwa, labda, alikosea," ama, "hilo lisingeweza kutukia katika siku hii." Lilionekana karibu haliwezekani wakati huo, lisilowezekana zaidi kuliko lilivyo siku hizi. Bali Mungu alilitimiza, haidhuru, kwa kuwa aliahidi ya kwamba angefanya jambo hilo.

57 Na hebu angalia jinsi anavyolifanya kwa urahisi. "Nimeshuka. Nilisikia kilio. Ninaikumbuka ahadi Yangu. Nami nimeshuka kuja kuitimiza, na ninakutuma wewe. Fanya hilo. Nitakuwa pamoja nawe. Hakika, nitakuwa pamoja nawe. Uninii Wangu usio-, Uwepo Wangu usioshindwa utakuwa pamoja nawe kokote uendako. Usiogope." Unaona? "Ninashuka kuja kukomboa." Nina hakika watu wa kiroho wanalishika hilo. Unaona? Unaona? "Mimi—mimi ni—mimi nitakutuma, kuwaleta watu Wangu kwenye kutoka. Kuwaita watoke, Nami nitakuwa pamoja nawe."

58 Sasa, jinsi—jinsi tunavyoweza kustarehe, jinsi imani inavyoweza kushikilia mahali hapo. Unaona? Mungu atafanya jambo hilo. Aliliahidi. Haidhuru vipi, hali ya mambo ikoje, ama yale asemayo mtu mwingine yeyote, Mungu atalitimiza, kwa vyovyote, maana Yeye aliahidi kulitimiza. Naye hulitimiza kwa urahisi sana, hata, li—linapitia juu ya u—ufahamu

wa watu walioelimika ambao wangejaribu kulitolea hoja, "Ingewezekanaje?"

59 Simaanishi kusema ya kwamba mtu sasa, mwenye akili nzuri, elimu nzuri, timamu, ya kwamba mtu huyo hatalielewa. Hiyo ni sawa, na nzuri sana, mradi tu anaitumia hiyo sio kwa kuhoji, lakini, elimu hiyo aliyo nayo, kumwamini Mungu. Hebu igeuzwe iwe ni urahisi wa kusikiliza yale aliyosema Mungu, na kuliamini. Elimu yake itamsaidia basi.

60 Angalia. Lakini mtu huyo anapojaribu kuhoji, "Isingewezekana," basi hilo linampeleka mbali na Mungu, sikuzote, wakati wote, wakati anapojaribu ku—kusikiliza kitu gani, ufahamu wake mwenyewe. Unaona? Kama hulipati, na Biblia inasema jambo fulani, liitikie tu, "Amina." Acha tu liende namna hiyo.

61 Sasa, badala ya kurejea kwenye Maandiko haya, unaweza kuyaandika chini kama kumbukumbu, katika somo hili la shule ya Jumapili. Lakini ningeninii, labda, kama mngetaka kuliangalia. Lakini, kwanza, nina mengi sana hapa. Hebu tu . . .

62 Kabla hatujapata kujua huku kutoka kunamaanisha nini, pia nitakufananisha huko kutoka sasa . . . kutoka wakati huo, na kutoka kwa siku hizi, na mwangalie kama haliendi sambamba. Kumoja ni kwa maumbile ya asili. Na mambo yale yale aliyofanya katika hali ya asili, Yeye analifananisha tena, analifananisha na jinsi ya kiroho, kutoka kwa kiroho.

63 Zuri mno, kuliona Neno la Mungu! Mtu yeyote angewezaje kusema halikuvuviwa? Hii ilikuwa ni karibu miaka elfu mbili na mia nane iliyopita, unajua. Na jinsi ambavyo Yeye aliahidi, na vile Yeye amefanya na kuliweka kule kama mfano, jinsi ambavyo Yeye—Yeye—Yeye anavyokifanya kivuli cha kitu fulani kushuhudia mambo yaliyo ha—halisi. Nitaliingilia jambo hilo, usiku wa leo, kati ya mwezi na jua, Bwana akipenda.

64 Lakini, kwanza, hatuna budi kuchunguza Mwanzo tuone ni kwa nini walikuwa huko Misri. Ni kwa nini watu wa Mungu wangekuwa nje ya nchi hiyo? Hata hivyo, Mungu aliahidi hilo, pale pale mwanzoni, pamoja na Ibrahimu, Isaka na Yakobo, huko Palestina, Mungu aliwapa nchi hiyo, na akasema, "Hii hapa." Loo, halafu, kwa nini watu wasiwe katika mahali walipopewa na Mungu?

65 Hilo ndilo swali la siku hizi, pia. Mungu alitupa pentekoste. Alitupa Kitabu cha Matendo. Alitupa Roho Mtakatifu, kutuongoza na kutuelekeza. Alitupa Nchi. Na ni kwa nini tumetoka Humo? Ni kwa nini kanisa limetoka Humo? Ni kwa nini kanisa kuu la Kikristo leo hii haliishi tena kama Kitabu cha Matendo, likileta kitu kile kile? Kuna sababu fulani kwa hilo.

66 Sote tunajua ya kwamba tumevurugika, na tuko katika hali mbaya sana. Na hali ya kuchukiza sana ambayo—ambayo Ukristo umewahi kuishi ndani yake, ni leo hii. Nasi tuko

kwenye...moja kwa moja kwenye kilele ama ukingoni mwa—mwa hukumu kuu mno ya kutisha, inayolikabili kanisa. Na kabla hukumu hii haijatolewa, Mungu anaagiza kutoka, kama tu vile alivyofanya wakati huo. Dhambi za Waamori zilikuwa zimelundikana, kwa hiyo Yeye—Yeye anaagiza ku—kutoka kwa kiroho. Sasa hebu na turudi nyuma kidogo, katika mfano, na tuone.

67 Walishuka wakaenda Misri, yote kwa sababu ya wivu wa ndugu mmoja. Hiyo ndiyo sababu kwamba Israeli walikuwa Misri wakati huo, nje ya nchi. Kumbukeni, ahadi za Mungu zilikuwa tu ni mradi walidumu kwenye nchi hiyo.

68 Sasa mnaweza kuona yale tuliyokuwa tukisema katika maombi, dakika chache zilizopita? Ni kwa nini ilimbidi Mungu kuufanya mgumu moyo wa Farao? Kuwarudisha watu katika ile nchi ya ahadi, kabla hajaweza kuwabariki, kuwaletea Masihi.

69 Ilimlazimu vipi kuufanya mgumu moyo wa Hitler, kuwachukia Wayahudi, wakati yeye, mwenyewe, akiwa ni nusu Myahudi? Aliwezaje kufanya jambo hilo katika Stalin, Mussolini? Unaona? Watu wasiovuviwa, kama taifa, wao—wao...Imembidi Mungu kuchukua vyo—vyombo wanavyoishi kwavyo, sheria za nchi, mara nyingi, kuzitimiza ahadi Zake. Kwa hiyo, ilimbidi kuifanya migumu mioyo ya hao watawala wa kimabavu, apate kumrudisha Myahudi katika nchi ya ahadi. Ilibidi iwe hivyo.

70 Sasa tunaona, ya kwamba, akishuka kwenda, Yusufu... Tunaijua hadithi hiyo, tunaporudi katika Mwanzo, nanyi mnaweza tu kuisoma. Kwa sababu, kidogo nimechelewa tu kuanza somo hili refu la shule ya Jumapili, na nitajaribu kuharakisha.

71 Angalieni sasa. Someni hadithi hiyo mtakapoweza, ya Yusufu, akizaliwa nyuma ya nduguze, karibu tu na yule wa mwisho. Watu wenye nia ya kiroho watalishika hilo sasa hivi. Yeye hakuwa mtoto wa mwisho; Benyamini alikuwa ndiye wa mwisho. Lakini, katika kule kufukuzwa, angalieni. Yusufu na Benyamini walikuwa ndugu wa baba mmoja na mama mmoja, na ndio wawili tu waliokuwa ni ndugu. Kamwe Benyamini hakutambuliwa mpaka alipokutana na Yusufu. Na juu ya wengine wote, Benyamini anapewa sehemu maradufu ya kila kitu alichotoa Yusufu. Vema. Angalieni sasa, tunaona kwamba kule chini, wao walikuwa...

72 Yeye alitolewa kutoka kwa ndugu zake kwa sababu kwamba alikuwa ni wa kiroho. Yeye alikuwa ni mtu mkuu, ingawa ndiye aliyekuwa mnyenyekevu kuliko wote wa kundi hilo, mdogo kuliko wote wa kundi hilo. "Nao walimchukia bila sababu." Hawakupaswa kumchukia. Walipaswa kumheshimu. Kwa sababu, ni kwa nini walimchukia, kwa sababu alikuwa ni ndugu? Siyo hivyo hasa. Walimchukia kwa sababu kwamba

Mungu alishughulika na yeye kuliko alivyoshughulika na hao wengine. Unaona? Alimpa u—u—u—ufahamu wa kiroho. Aliweza kufasiri ndoto, kikamilifu. Na aliweza kutabiri mambo ambayo yangekuja kutimia, kikamilifu, jinsi hasa yalivyokuwa. Wala yeye—wala yeye hakucheza.

73 Yeye aliona ndo—ndoto ya ile miganda ikisujudu mbele ya miganda yake, na hapo ndugu zake wakamkasirikia. Kasema, "Nadhani, basi, ewe maskini mtakatifu anayejifingirisha," kwa maneno mengine, "ati itatulazimu kusujudu mbele zako siku moja?" Lakini hivyo ndivyo ilivyotukia. Unaona? Hayo majitu makubwa yangaliwezaje kusujudu mbele ya maskini jamaa huyo mdogo, asiye chochote aliyekuwa anasimama pale? Lakini walifanya hivyo, hakika walisujudu, na wakaomba rehema. Lakini hakuwa ameingia mamlakani, bado, unaona. Wakati huo alikuwa tu utotoni.

74 Na ndipo tunaona, kwa kufanya jambo hili, kwamba Yusufu aliondolewa miongoni mwa ndugu zake, madhehebu, na kuwekwa peke yake. Unaona? Ndugu zake, wote humo nchini. Na halafu kukaja jambo kubwa sana. Tunatambua ya kwamba Israeli . . . mradi tu walidumu mahali pao, na kuendelea. Sasa, hilo ni jambo moja zuri, kukaa mahali hapo. Mahali pao, hilo ni sawa. Lakini, walimwondosha Roho.

75 Watu wa kimsingi, leo hii, wanajua mahali pao kwamba wao ni akina nani, kwa dhana za kiakili za Biblia, bali hakuna Roho. Wamemkataa Yusufu, wamemfukuza. Hawakutaka uhusiano wowote na jambo Hilo. "Ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Ni ninii . . . Hatutaki uhusiano wowote na Hilo." Wamemfukuza, wamemuuza, kwa ulimwengu. Walikuwa wametoka kwenye ushirika wao.

76 Sasa, kwa kufanya jambo hilo, walikuwa wanaondoa kutoka mahali pake, wakapelekwa Misri, baadaye.

77 Sasa, hadithi ya hawa ndugu wenye wivu hakika ni mfano mkubwa wa upande wa kiroho siku hizi. Sisi—sisi sote tunajua jambo hilo, ya kwamba ni wivu safi, sio safi. Ni maskini wivu wa kale, mchafu, wenye kinyaa. Unaona? Hakuna usafi katika wivu. Unaona? Si kitu ila wivu mchafu. Wakati, wanaiona Biblia ile ile, na tabia ya Mungu yeye yule aliyeiandika Biblia, akijithibitisha Mwenyewe, na kisha wanalikataa Hilo bila sababu. Safi . . . Vema, sio safi. Kama nilivyosema, ni wivu mchafu. Wanamwangalia Mungu akiwaponya wagonjwa, akiwafufua wafu, Mungu yeye yule aliyeishi katika siku za mitume! Injili ile ile waliyoiandika, kwa ajili ya safari hii ya kiroho, ni Mungu yeye yule anayefanya jambo lile lile. Kwa hiyo wao si kitu ila wivu, wamemfukuza, "Wala hatutakuwa nalo miongoni mwa watu wetu." Unaona? Wakawafukuza!

78 Waliwazia, hao ndugu, ya kwamba mtu kama huyo asingewafaa kitu, kwa hiyo, "Kwa nini tusimwondoe tu?"

79 Hilo ndilo, jambo lilo hilo limetukia siku hizi. Wao wanadhani, ya kwamba, "Kwa kuwa kwamba makanisa yetu yamekuwa ni ya kielimu, kwamba tuna umati uliovalia nadhifu kuliko wote, dhehebu lililo kubwa kuliko yote, wahudumu wenye akili kuliko wote, kwamba hatuna haja ya Roho Mtakatifu jinsi kama alivyokuwa huko nyuma." Kwamba, wao wameshiba. Kwa maneno mengine, matendo yananena kwa sauti kuu kuliko maneno: Kwamba seminari zao, na ninii zao. . .akili za utu wa—wao, na kukusanyika kwao na—na kulijadili jambo hili, wanaweza hata na zaidi, kwa akili zao wenyewe za kielimu, kuliweka Kanisa katika utaratibu, vizuri zaidi kuliko vile Roho Mtakatifu angaliweza kufanya. Kwa hiyo, hawamhitaji tena. "Ni kitu ambacho hatukihitaji siku hizi. Ni, ni cha siku zilizopita." Sasa, hivi hilo si ni kweli tu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Hatumhitaji Roho Mtakatifu kuwaponya wagonjwa. Tuna madaktari. Hatumhitaji Roho Mtakatifu kunena kwa lugha. Sisi sote tu watu wenye akili." Na unapofanya hivyo, unaondoa, papo hapo kutoka kwenye mwili wako, Tegemeo la maisha.

80 Yesu aliwaambia hao Wayahudi, katika siku Zake, "Hivi hamjasoma ya kwamba, 'Jiwe lililokataliwa ndilo Jiwe kuu la Pembeni ambalo jengo lote linakalia'?"

81 Sasa, mnaona ninalomaanisha? Nina hakika m—mnaweza kushika jambo hilo. Hiyo, sa—sababu yake sasa, ni kwa sababu walidhani kamwe hawangemhitaji. "Hatuwahitaji wanena kwa lugha. Hatuhitaji wafasiri wa lugha. Hatuwataki tena manabii wa Agano la Kale kutuweka katika utaratibu, kwa Roho Mtakatifu. Tunafahamu Hilo." Unaona? Wamechukua mfumo wa kujibunia kupachukua mahali pa Roho Mtakatifu.

82 Kwa hiyo, kuna watu walioteuliwa, walioandikwa majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, hawawezi kuliendea jambo hilo. Wao wana nia ya kiroho, na kwa hiyo hawawezi kuliendea jambo hilo. Hawawezi kulivumilia, haidhuru kama baba na mama zao waliishi katika kanisa lolote lile la kimadhehebu.

83 Wakati kanisa linapotenda, linapofanya, labda halitasema hayo moja kwa moja. Lo, la. Hawatalisema wazi wazi, bali matendo yao yanathibitisha hilo. *Hili* hapa Neno. Na Roho Mtakatifu analithibitisha miongoni mwa hao, wakati anapoweza kuwakusanya pamoja, ya kwamba angali anawaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu, na kunena kwa lugha, na kutoa pepo. Kwa hiyo, inategemea ninii . . . kilicho ndani ya mtu.

84 Bibi Arganbright pale, alikuwa akiwazia hilo, hivi majuzi, akiwa ameketi pale njiani, aking'oa nyasi kidogo, wakati alipokuwa akikata nyasi uwanjani. Nilipitia pale, karibu sana naye. Hakunitambua, nami nikamwacha tu aendelee. Nilikuwa nikiangalia.

Sasa mwangalie Roho Mtakatifu katika kazi Yake kuu.

85 Kanisa linajisikia ya kwamba halimhitaji Roho Mtakatifu. Makanisa yatakwambia hilo. Na watu hao wanaweza kusimama na kukupa mazungumzo mazito sana ya kielmu, karibu wanaweza kukufanya uamini hilo. Sasa hebu na tusimame hapo, kidogo. Je! hivi Yesu hakusema ya kwamba hizo mbili zingefanana sana, "Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mahubiri ya kiakili yangekuwa ya kuvutia sana, hata yange—yangewapoteza watu. Ni injili, ni watu wanaoweza kulitumia neno hilo hivi kwamba, hata karibu angemfanya mtu yeyote msomi, kama unatumainia tu akili zao, wa—wangemkataa Roho Mtakatifu, na—na kuichukua njia ya mwanadamu. Tunaona jambo hilo.

86 Sasa, hilo ndilo jambo lile lile walilowazia juu ya Yusufu, nao wakamwondoa. Na, loo, huko Misri, loo, jinsi tunavyoweza kuwazia, jinsi ambavyo ningeweza kutumia saa nyingi. Ungeweza kukaa hapa kwa miaka mitatu wala usiondoke kwenye somo hilo, usiku na mchana, na bado uwe ungali unapata uhondo wa Roho Mtakatifu. Mtu wa kiroho anaweza kuangalia huko Misri na kuona yale mateso yakiibuka; anaweza kumwona Yusufu akiondolewa, kusudi mateso yaweze kuibuka. Na kisha amwone Mungu, akiwa na gurudumu Lake katika magurudumu, kila kitu kikizunguka kikamilifu tu. Amwone Potifa akimkataa Yusufu; aone ule uongo ukisemwa. Na kumwona Yusufu gerezani, na ndevu zake zimekua, amekataliwa na ndugu zake. Lakini basi, mara, Mungu akaingia. Unaona?

87 Jinsi tunavyoweza kuona lile gurudumu ndani ya magurudumu, likisonga! Mpango mkuu wa Mungu ukisukuma kila kitu kuelekea kwenye huku kutoka, kwenye wakati huu ambapo Yeye angewaita watu wake warudi nchini tena, warudi mahali pale, mahali pao ambapo Yeye angeweza kuwabariki na kumweka miongoni mwao Yule ambaye Yeye aliahidi angemweka miongoni mwao. Ilibidi wawe katika nchi yao. Kumbuka, ilibidi watoke kwenye nchi waliyokuwamo na waingie kwenye nchi ya ahadi, kabla ya kuja Kwake Masihi wao aliyeahidiwa.

88 Nalo kanisa halina budi kufanya jambo lile lile; litoke kwenye kundi hilo la wanaokataa, waingie kwenye ile ahadi, kabla Masihi hajapata kudhihirishwa mbele zao. Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Maisha ya Masihi, yakidhihirishwa, kulifanya Kanisa tayari, Bibi-arusi.

89 Mwanamke akiolewa na mwanamume, na kupingana naye, ingekuwa ni namna fulani ya m—mzozo, daima. Lakini wakati mwanamume na mkewe, mpenzi wake msichana, aliyemposa, wakati wakiwa katika upatanifu mkamilifu, kama vile nafsi moja na moyo mmoja, kwa sababu watakuwa ni mwili mmoja.

90 Ndipo, wakati Kanisa linapoweza kupata upatano wa jinsi hiyo pamoja na Mungu, mpaka dhihirisho la Bwana-arusi

limedhihirishwa katika Bibi-arusi, kwa maana watakuwa ni mmoja! Loo, ni somo kuu jinsi gani. Vema.

91 Sasa, kumbukeni, mtu wa kiroho akichukua jambo hili, anaweza kuona mfano wake na kile kilichofananishwa, na kuuchukua. Kwa wakati mmoja, ninii tu, tungeweza kuendelea saa nyingi nalo. Angalia jambo linalotukia.

92 Na ni kwa nini tumengojea miaka hii yote, tangu oasisi hii ya wakati? Mnajua, Biblia inasema, ya kwamba, "Kanisa lilikimbilia nyikani, ambako lililishwa kwa wakati na wakati." Basi ni kwa nini haya yote yametokea? Kwamba sisi . . . .Mnaona? Yangali ni magurudumu ya Mungu ndani ya magurudumu.

93 Kwa nini Mungu hajafanya jambo hili, muda mrefu uliopita, wakati wanaume waliketi chini na penseli, na—na wanawake, na kujaribu kuuchora tu wakati huo? Kama vile Hakimu Rutherford na wengi wao, ya kwamba, "Yesu atakuja mwaka wa '14." Na—na Mama Shipton alikuwa amekupangia mapema zaidi ya hapo, na kadhalika, nyakati hizi zote. Na, mnaona, wakifuatilia hili, kwa yale waliyokuwa wameyawazia kutokana na Maandiko, mnaona, waliliharibu. Limefichwa. Kwa kweli limefichwa. Na Maandiko yangewezaje kujipinga, wakati Yesu alisema, "Hakuna mtu anayeijua ile dakika ama saa"? Unaona? Unaona? Wanachukua tu sehemu moja ya Maandiko na kuishikilia.

94 Inakupasa kuchukua Kitu hicho chote. Halafu, kama Mungu yumo kwenye hilo, basi Mungu atadhihirisha hilo kwamba ni Kweli. Kama vile uponyaji wa Kiungu, kama si wa Kweli, basi si wa Kweli; Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nao. Lakini kama akiudhihirisha kuwa ni Kweli, basi ni Kweli. Kama tu vile Yesu . . .

95 Mungu alisema, "Akitokea kati yenu, nabii, ama wa kiroho, nitasema naye. Na yale asemayo yakitimia, basi yasikieni. Jambo ndilo hilo. Lakini kama unabii huo si wa kweli, basi . . . " Mungu hawezi kukosea. Yeye hana kikomo, hawezi kukosea, ni mwenye nguvu zote, wala hawezi kukosea. Kwa hiyo, kama mtu huyo ndiye anayenena, basi inaonyesha mtu huyo. Kama alisema maneno yake mwenyewe, yatakosea. Lakini kama akinena Maneno ya Mungu, hayawezi kukosea, kwa maana Mungu Ndiye anayenena. Basi, uvuvio wake unatoka kwa Mungu, nao utaninii . . . hauna budi kabisa kuwa ni wa kweli. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema ujulikane. Hivyo ndivyo Bi- . . .

96 Katika Agano la Kale, Yeye alisema, "Ikiwa hawaneni sawasawa na sheria na manabii, ni kwa kuwa hawana Uzima ndani yao, hawana Mwanga ndani yao." Kweli. Inawabidi kunena sawasawa na sheria na manabii. Na unabii, ama chochote kile, hakina budi kilingane na Neno. Kama sivyo, ni cha makosa. Mnaona?

97 Sasa, tunaona ya kwamba mambo haya yote yametimia, kwa sababu, tulingojea. Miamsho: Wamethodisti, Walutheri, Wabaptisti, Wakampbeli, na—na wote mbalimbali. Wamekuwa na miamsho mikuu. Mnazarayo, Mpilgrim Holiness, Wapentekoste, wote walikuwa na miamsho mikuu. Bali kule kutoka kukuu hakukuwa kumetukia bado. Kwa nini? Mungu alimwambia Ibrahimu angemweka nchini wakati uo huo, bali u—uovu wa Waamori haukuwa umetimia bado. Na Mungu amengojea, kwa subira. Hao watu, wakijaribu kukisia, wanaweza kuyaona Maandiko yakiingia moja kwa moja kwenye jambo fulani. Yanaingia moja kwa moja katika kitu fulani, wao wakasema, "Siku ndiyo *hii*. Wakati ndio *huu*." Bali mnashindwa kufahamu ya kwamba uovu wa Waamori haujatimia bado.

98 Miaka mia nne wangekuwa wasafiri kule Misri, na kisha watolewe. Lakini kwa kweli walikaa miaka mia nne na arobaini, kwa sababu ya kumkataa nabii. Iliwabidi kuteseka kwa mingine, karibu miaka arobaini kule chini nyikani, kabla Mungu hajawatoa. Musa alikuwa huko nje nyikani miaka arobaini kabla hajapata kurudi kuwakomboa, unaona. Miaka arobaini ilikuwa ni ya ziada, ilipita, kwa kuwa waliukataa ujumbe.

99 Sasa, miaka arobaini katika wakati wa Mungu ingekuwa ni kama dakika moja na nusu, kwa wakati wetu. Hivyo ndivyo ilivyo tofauti. "Miaka elfu moja ni siku moja tu." Unaona? Hata isingekuwa ni dakika moja, hata kidogo. Angalia, kwenye jambo hilo.

100 Sasa tunachelewa. Kwa nini? Mungu amekuwa akivumilia, akingojea, akitazamia. Aliwaacha Wa—Walutheri wainuke katika uamsho, kisha wakaunda dhehebu. Akawaacha Wamethodisti wakainuka katika uamsho; wakaunda dhehebu. Akamwacha John Smith, kanisa la Kibaptisti, liinuke kwa uamsho mkuu; likaunda dhehebu. Akawaacha Wapentekoste wainuke kwa kurudishwa kwa vipawa; wakaunda dhehebu. Mpaka uovu utakapojaa kabisa, ndipo Mungu amechoka, ndipo kutoka kunakuja.

101 Na tunaliona, ya kwamba watu wenyewe wanaweza kuona huko nyuma kwenye mtiririko wa wakati, kwamba kitu hicho kimelaaniwa. Wanachukua kabari na joho zuri la Kibabeli, tena. Na hicho ndicho kitu kinacholaani miongoni mwa watu, wakati watu wanapojaribu kuingiza mawazo yake mwenyewe kuhusu mambo.

102 Hatuna budi kudumu na hilo Neno. Hizo ndizo amri za Mungu, zilikuwa, "Msiguse chochote kwenye mji huo, mji huo uliolaaniwa. Msikiguse. Kiacheni."

103 Naye Akani alifikiri angeweza kuchukua kabari hii ya dhahabu na aishi vizuri sana kama walimwengu wengine, na joho zuri la Kibabeli. Loo, kwa akina Akani kambini! Unaona? Lakini kitu hicho kimelaaniwa, na daima kimelaaniwa.

Kililaaniwa tangu lile Baraza la Nikea lenyewe, hapo Nikea, Roma, kimelaaniwa tangu wakati huo. Lakini Mungu ameuacha uovu utimilike, mpaka wakati wa Waamori utakapokuwa karibu kutimia.

104 Na sasa mtu yeyote mwenye ufahamu wa kiroho, kumbukeni, ninaendelea kunukuu, ufahamu wa *kiroho*, unaweza kuona ya kwamba uovu wa taifa hili umetimia. Limejiundia madhehebu na kuunda tena, na kuunda tena na tena. Na sasa limeunganishwa, na linaungana na kitu kingine. Uovu umetimia. Wakati wa kutoka umewadia, wakati wa kuitwa tutoke, tuingie kwenye Nchi ya ahadi. Sio ahadi, nchi nyingine tu ya kuendea; bali ni Nyumbani, ule Utawala wa Miaka Elfu, wakati wa kuitwa tutoke. Uovu wa taifa hili (nitaligusia tena usiku wa leo, Bwana akipenda) umetimia. Ni kinyaa.

105 Mnasema, "Ndugu Branham, ati taifa unamoishi wewe?" Naam, bwana. Hakika. Unasema, "Kama raia wa Marekani, haikupasi kusema jambo hilo." Basi, Eliya asingepaswa kuilaani Israeli, na yeye akiwa ni Mwisraeli basi. Hao manabii wengine hawakupaswa kulilaani taifa hilo walilokuwa Waisraeli chini yake.

106 Lakini walinena tu, sio mawazo yao wenyewe, bali Neno la Bwana. Unaona? Inategemea unakotoa uvuvio wako. Inategemea jinsi unavyokuja. Kama ni kinyume na Neno, achana nao. Ninamwalika mtu yeyote kuthibitisha ya kwamba huo ni kinyume na Neno.

107 Je! Biblia haikusema, katika Ufunuo 13? Hapo ndipo taifa hili linapoonekana. Taifa hili ni namba kumi na tatu, taifa la mwanamke. Ni mwanamke, katika Biblia. Mwanamke yuko kwenye sarafu zetu. Ni taifa la mwanamke. Ndiko uozo wa wanawake ulikoanzia, unakoanzia, ndiko unakoishia. Uozo ulianzia Edeni, kwa kutokuliamini Neno la Mungu. Hapa ndipo lilipowaangulia wahubiri wanawake na chochote kile. Uchafu wa ulimwengu unatoka moja kwa moja Hollywood, taifa lililo baya zaidi ulimwenguni; talaka nyingi zaidi, kuliko za ulimwengu mzima ukiwekwa pamoja. Unaona? Kwa nini? Mtaona moja ya siku hizi, Bwana akipenda. Mtaona ni kwa nini, kitu hiki kilicholaaniwa. Mnaweza kuona upofu wa upuuzi huu wa talaka ambao Shetani ameufunika juu ya macho ya watu. Tuko katika saa ya hatari. Mwisho wetu uko karibu sana sasa, ninaamini. Wameoza, wameoza mpaka kwenye shina.

108 Linaonekana katika Ufunuo 13, namba kumi na tatu. Pia kumbukeni, liliinuka kama mwana-kondoo, uhuru wa dini. Lakini baadaye lilipokea mamlaka kutoka kwa yule mnyama; sanamu kama yake. Nalo likanena kwa mamlaka yote, na kufanya mambo yale yale maovu ambayo yule mnyama alifanya mbele yake. Kisha mnaniambia ati hayajatabiriwa kuhusu taifa

hili? Hali ya Waamori iko karibu kuiva, kwa maana tayari wanatenda kazi ndani yake.

109 Na hata papa wetu mpya, kusudi lake kuu ni kuwaunganisha ndugu pamoja. Na, kwa jicho la kawaida, ndilo jambo la kufanya. Lakini, mbele ya macho ya Mungu, ni kinyume na Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuchanganyikana na hayo. Na kila kanisa litaitwa liingie kwenye muungano huo. Tokeni kwenye kitu hicho, upesi mwezavyo. Mtaichukua alama ya mnyama, bila kujua mnalofanya. Tokeni kwake.

110 Ninatumaini mtu wa rohoni anaweza kulishika hilo. Nina hakika mnalishika. Lakini sijui, huko nje. Kwa vyovyote vile, huwezi kutembelea kila taifa. Unaweza kutuma kanda huko. Mungu atakuwa na njia fulani ya kumshika mtu huyo huko nje ambako mbegu hiyo inapandwa. Kweli. Na mara Nuru itakapoigusa [Ndugu Branham anapiga makofi yake mara moja—Mh.], imetoka, imepata Uzima. Kama vile yule mwanamke pale kisimani, alisema, "Hilo hapo." Akaishika.

111 Tokeni kwenye kitu hicho. Kimelaaniwa. "Ati kimelaaniwa?" Niambieni ambapo moja lilianguka na likainuka tena. Niambie moja ambalo lilipata kuinuka ambalo halikuanguka. Kwa hiyo, unaweza kuona ya kwamba kitu hicho ni makosa. Vema.

112 Uovu haukuwa umetimia bado, wa Waamori, kwa hiyo ilibidi wakawie na kungojea kabla ya kule kutoka. Lakini wakati Waamori walipoutimiliza uovu wao, ndipo kukaja kutoka kwa kiroho, ama kutoka kwa kawaida, kuwapeleka watu kwenye nchi ya kawaida, ambako Mwamori wa kawaida alikuwa ameishi wakati mmoja, wakaiita hiyo kuwa ni nchi yao.

113 Na uovu wa dhehebu la Kimwamori wamejiita wenyewe "Kanisa," kwa muda mrefu sana, mpaka uovu wao uko karibu kutimia.

114 Kunakuja kutoka, ambako Mungu ataonyesha nani ni nani; ambapo Kanisa lenyewe, Bibi-arusi wa Yesu Kristo, atatolewa nje, aingie kwenye Nchi iliyoahidiwa. "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi, katika mahali hapa." Haikubidi kwenda Huko na kupigana kama walivyopigana. Yameandaliwa tayari. Kama maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja inayongojea tayari, "Ili nilipo Mimi, hapo ninyi pia mtakuwapo." Kule kutoka kukuu kumekaribia!

115 Angalia jinsi Mungu alivyokufanya kutoka huko, kile Yeye. . .yale matayarisho aliyofanya, na uyachunguze kwa dakika moja, kisha uangalie siku hizi. Vema. Angalieni, kabla ya huku kutoka, "Paliinuka fa—farao asiyemjua Yusufu." Unaona? Farao asiyemjua Yusufu. "Hakumjua Yusufu." *Yusufu* aliwakilisha nini? Sehemu ya kiroho katika kutoka huku kwa kiroho.

116 Kunainuka sasa, "Sisi ni uhuru." ("Yule mwanamke alilishwa kwa wakati, wakati, na nusu wakati.") Lakini

hatimaye paliinuka Yu—Yusu-. . .ama farao mtawala wa kimabavu asiyejali uhuru wa dini, akiwaunganisha pamoja. Msiache jambo hilo liwapite. Kulikuja wakati ambapo kulikuwako na farao, kwanza, ilibidi aje.

117 Nayo madhehebu yaliishi kwa anasa kuu, yaliishi kama tawi lililopandikizwa, kwenye mzabibu halisi wa Ukristo, bali lingali linazaa matunda yake ya asili; wanawake, nusu uchi; wanaume, kielimu, na wakikana nguvu za Roho. Lakini, limeishi chini ya jina la kanisa la Kikristo. Ni mzabibu uliopandikizwa. Lakini Mkulima anakuja sasa kuupogoa huo mzabibu, kama alivyosema angefanya. Wote hao wasio na tunda wanakatiliwa mbali na kutupwa motoni na kuteketezwa.

118 Ni jambo la kuogofya sana kusema, bali Kweli wakati mwingine inaonekana inatisha sana, kama nilivyowaambia sasa hivi, jinsi ambavyo Mungu huwapitisha watoto Wake kwenye maji yenye kilindi na matope ya mchanga na kadhalika. Yeye hufanya jambo hilo hivyo. Kumbukeni, nyu—nyungu haina budi kuvunjiliwa mbali ikawa vigae, matita, vipande vidogo vidogo vipate kufinyangwa na kusagwa tena. Linaonekana kama ni jambo baya sana kuiangamiza, bali inabidi ifanywe hivyo, kusudi nyungu hiyo iumbike tena, jagi ama chochote kile unachoumba.

119 Kulikuwa na farao aliyeinuka, ambaye hakumjua Yusufu." Na huo ulikuwa ndio mwanzo wa mwanzo. Huo ulikuwa ndio mwanzo wa kule kutoka. Na wakati kitu hicho kilipoanza kuumbika, chini ya nguvu za si—siasa, kilipoanza kuumbika, Mungu alianza kujiandaa. Uovu wa Waamori ulitimia. Wakati aliomwahidi Ibrahimu ulitimia, na wakati wa ukombozi ulikuwa umekaribia.

120 Na Mungu akamruhusu farao kuinuka, ambaye hakumjua Yusufu, na Ramesesi akazaliwa. Na moja kwa moja baada ya Seti akaja Ramesesi. Na Ramesesi alikuwa ni yule ambaye hakuzijua zile baraka za Yusufu. Wala—wala hakujua upande wa kiroho ulivyokuwa. Yeye alikuwa tu ni mtu mwenye kipaji cha siasa, kwamba angeweza kuiteka Ethiopia na nchi hizo zingine zote, chini ya nguvu za kijeshi. Na hilo tu ndilo alilojua, lilikuwa ni nguvu za—za kijeshi.

121 Na ninafikiri, kama mtu yeyote alikuwa ni wa kiroho, angeweza kuona yale yanayotukia sasa. Tunampata farao asiyejua uhuru wa dini. Wakati rais wetu alipotawazwa, hangeweza kuliapia jambo hilo, ya kwamba aliamini katika uhuru wa dini.

122 Vipi kuhusu hivi majuzi wakati tulipokuwa na suala hili la ubaguzi, huko Kusini? Wakati gavana huyu wa—wa Alabama. . .laiti ningaliweza kuzungumza na mhudumu huyo, yule Martin Luther King. Mtu huyo anawezaje kuwa kiongozi, na anawaongoza watu wake kwenye mtego wa mauti? Kama watu

hao wangalikuwa ni watumwa, ningekuwa kule chini, nimelivua koti langu, nikiwapigania watu hao. Hao si watumwa. Ni raia. Hao ni raia wa taifa hili. Suala la “kwenda shuleni.”

123 Hao watu, kama wana moyo mgumu wala hawajui mambo hayo. Huwezi kusokomeza ndani ya watu, mambo ya kiroho, kile kilichoingizwa mle kwa nguvu za kisiasa. Hawana budi kukubali jambo hilo, wazaliwe mara ya pili, ndipo watayaona mambo haya.

124 Lakini, mtu huyu, laiti ningaliweza tu kuzungumza naye; akiwaongoza watu hao wa thamani, chini ya jina la dini, kuingia kwenye mtego wa mauti ambako atawaua maelfu mara maelfu yao! Hawaninii . . . Wao wanapata tu upande wa ki—kimwili.

125 Mtu huyu, yule ndugu mweusi, wakati yale maasi makuu yalipotukia huko Louisiana, nilikuwa huko wakati huo. Wakati ninii . . . Kulikuwa na mhudumu mweusi, ndugu mzee wa thamani, aliyesimama hapo na kusema, akawaomba wanajeshi, “Je! ningeweza kuzungumza nao? Hao ni watu wangu.” Na mzee huyu mhudumu akasimama, hapo, kasema, “Ninataka kusema, asubuhi ya leo, sijapata kamwe kuionea rangi yangu aibu. Muumba wangu aliniumba kile nilicho.”

126 Hivyo ndivyo anavyomtaka abaki. Hivyo ndivyo anavyomtaka kila mtu kubaki. Yeye huumba maua meupe, na maua ya bluu, na maua ya kila rangi. Usiyazalishe na mengine. Usiyazalishe kwa kuchanganya mbegu. Unakuwa kinyume na maumbile.

127 Alisema, “Kamwe sijapata kuionea aibu rangi yangu, mpaka asubuhi ya leo.” Akasema, “Wakati ninapowaona watu wangu wakiinuka na kufanya mambo wanayofanya sasa,” akasema, “inanifanya niwaonee aibu.” Ee Mungu, ibariki sauti hiyo. Akasema, “Mtasababisha tu vurugu.” Kasema, “Angalieni shule zilizopo hapa. Kama tusingalikuwa na shule,” kasema, “ingekuwa ni jambo lingine. Lakini ni nani walio na shule nzuri zaidi hapa Louisiana?” Kasema, “Hebu tuchukue, kwa mfano, mji wetu, Shreveport.” Kasema, “Kuna shule ya wazungu kule, ni shule ya zamani. Walitujengea nyingine. Hawana hata zana moja, kitu kimoja cha kuchezea watoto. Tuna uwanja mzima uliojaa. Na mbali na hilo, walitujengea bwawa kubwa mno la kuogelea la marmar kwa ajili ya watoto wetu. Pia tuna waalimu walio bora sana wanaoweza kupatikana.” Kasema, “Kwa nini mnataka kwenda kule, wakati tuna iliyo bora hapa? Mna shida gani?” akasema.

128 Na hao watu, wao, “Heko!” Waliinyamazisha sauti hiyo. Haya basi, unaona, uvuvio mbaya.

129 Hao watu walikuwa ni watumwa. Wao ni ndugu na dada zangu. Wangalikuwa watumwa, ningesema, “Hebu na tujiunge nao na tushuke twende mtaani na kupinga kitu hicho.” Wao si watumwa. Wao ni raia wenye haki zile zile alizo nazo mtu yeyote

mwingine. Ni lundo tu la uvuvio unaotoka kuzimu, kusababisha milioni yao kuuawa. Wanaanzisha mapinduzi. Hakika, ndivyo ilivyo. Si haki.

130 Wanaume na wanawake wana haki zao wenyewe. Ndugu zetu weusi, na Wajapani wetu, na wa manjano, weupe, weusi, na chochote walichokuwa, hakuna tofauti katika rangi yao, kwa Mungu. Sote tunatoka kwa mtu mmoja, Adamu. Lakini kama Mungu alitutenganisha na kutufanya rangi tofautitofauti, hebu na tubaki hivyo. Kama ningalikuwa mtu wa ma—manjano, ningetaka kubakia Mjapani, ama Mchina. Ningalikuwa mtu mwe—mwe—mweusi, ningependa kubaki hivyo. Mungu aliniumba hivyo.

131 Kwa kweli, kuna mambo mengi sana kuhusu jamii ya watu weusi ambayo jamii ya wazungu inapaswa kuwa nayo. Hawana wasiwasi. Wao ni wa kiroho zaidi. Kuna maelfu ya mambo juu yao ambayo mzungu hata hawezi kuyagusa. Mungu aliwaumba hivyo.

132 Ni nani angaliweza kuimba kuliko kwaya ya watu weusi? Ungepata wapi sauti? Nimewaona wakitoka kwenye nchi huko nyuma, hawakujua ni upi, mkono wa kulia na wa kushoto. Makabila thelathini ama arobaini yao, nao wanaimba kufikia mahali, wanamuziki wanasimama pale, wanasema, "Kamwe siwezi kuigusa." Alifunza kwaya nyingi kwa miaka mingi, na mmoja angekuwa sauti ya nane ya juu, na ya chini, na kila kitu. Kasema, "Usikilize huo, mkamilifu kabisa, hata katika lugha tofauti." Wana kipaji.

133 Lakini, unaona, upuuzi huu wote hauna budi kutukia, yote kwa sababu ya mwanasiasa ambaye ninyi watu mlimchagua kwa mitambo yenu midanganyifu.

134 Na hivi majuzi, wakati yule gavana aliposimama pale, akaapishwa na kuchaguliwa mamlakani, na watu, na suala la ubaguzi kulingana na katiba ni, ya kwamba kila—kila mkoa unaweza kuchukua wazo lake wenyewe kuhusu jambo hilo. Yeye hakujali, bali aliisoma katiba, kasema, "Sasa, shule inatetea ubaguzi." Wana shule kule. Na ni watoto wawili tu weusi waliotaka kuingia kwenye shule hiyo, wakati wakiwa na chuo chao wenyewe. Bali alisimama na kusema, "Ati nini?" Hata aliisoma katiba.

135 Ndipo lilipomrudia jamaa huyu tuliye naye hapa juu, asiyemjua Yusufu, uhuru. Akizivutia hizo kura za watu weusi, na bila kujua chama cha kijamhuri ndicho kilichowaweka huru, kwanza kabisa. Wakiuza haki zao za mzaliwa wa kwanza, kwa kitu kama hicho, kiwaongoze kwenye mtego wa mauti, kuonyesha ya kwamba kila mfumo wa kujibunia hauna budi kuanguka. Kweli kabisa. Na Bw. Kennedy akataifisha ulinzi huo, na kuwatuma watu hao mbele ya baba zao wenyewe waliosimama pale chini ya katiba. Hilo lilikiuka katiba tena.

136 Kasema, "Hatutapigana. La, bwana." Kisha kasema, "Natumaini taifa hili linaweza kujua kwamba hatuishi tena chini ya demokrasia, bali chini ya utawala wa kiimla wa kijeshi."

137 Mnajua ule msemo wa kale, "Ukiisha kuwa mwanademokrasia wa kusini, daima utakuwa hivyo." Sijui sasa. A-ha. Hakika mtu atakuwa na akili ya kutosha kuamka kwa jambo fulani. Unaona? Waacheni watu hao wa thamani. Msiwaue, huko chini.

138 Kama yule jamaa aliyempiga risasi yule ndugu mgongoni, hivi majuzi usiku, kwa bunduki ile, na watoto wake wadogo na mkewe wakiwa ndani ya nyumba. Sijali yeye ni nani, hilo ni jambo la kishenzi na duni. Naam, bwana. Ningependa kuwa hakimu kwenye kesi hiyo, wakati mmoja. A-ha. A-ha. Kumpiga risasi mtu huyo, akija nyumbani kwa mkewe na watoto wake. Yeye ni raia, ana haki ya kutetea yale anayofikiria ni haki, mtu wa thamani. Picha kwenye gazeti la *Life*, yule mvulana mdogo akimlilia baba yake. Na mhuni fulani huko nje, amempiga risasi mgongoni, kwa kumvizia.

139 Hayo ndiyo unayoyapata unapomkataa Kristo. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo taifa zima limefikia, lote chini ya siasa. Ni aibu sana, bali hilo ndilo tulilotaka. Tulithibitisha jambo hili kwenye uchaguzi huu.

140 Mwanangu mdogo aliniambia, asubuhi ya leo, "Baba, wale wazee wetu wasafiri, walipokuja hapa, je! wote walikuwa ni wafuasi wa dhehebu *hili* fulani la kanisa? Je! wote walininii . . . " Kasema, "Walivaa makabuti makubwa?"

141 Nikasema, "La, mpenzi. Walikuja hapa kwa ajili ya uhuru wa dini. Hilo ndilo lililowaleta hapa, kuondokana na upuuzi kama huo." Unaona mahali limefikia sasa? Inaonyesha falme hizi zote hazina budi kuanguka.

Sina budi kuharakisha.

142 Jambo moja, ninaomba ya kwamba Ndugu Martin Luther King hivi karibuni ataamka. Yeye anawapenda watu wake; hapana shaka. Lakini kama tu akiona mahali ambapo uvuvio wake ulipo. Ingekufaa nini kama ulienda shuleni, milioni moja yenu mmelala huko, mmekufa? Usingeninii tu, ungeenda shuleni, hata hivyo? Sasa, kwa—kwa ajili ya njaa, kama ilikuwa ni kwa ajili ya kitu chochote kingine, watumwa, mtu huyo angekuwa ni mfia imani kuyatoa maisha yake kwa ajili ya jambo kama hilo, kusudi linalofaa, na hilo lingekuwa ni kusudi linalofaa. Lakini kuenda tu shuleni, mimi—mimi silioni. Unaona? Sidhani Roho Mtakatifu anakubaliana naye, hata kidogo, juu ya jambo hilo. Limewachochea watu vibaya sana, katika lundo la fujo, unaona.

143 Kama—kama tu Hitler alivyofanya, huko Ujerumani, aliwaongoza moja kwa moja kwenye mtego wa mauti, hao

Wajerumani wa thamani. Nao wakalala kwa mabilioni, ama mamilioni, wamelundikwa kule mmoja juu ya mwingine.

144 Na hilo ni jambo lile lile hasa. Na kumbukeni, niko kwenye kanda. Mtaona jambo hilo, baada, labda baada ya mimi kuondoka. Hilo ndilo litakalotukia hasa. Hao watu wa thamani watakufa kule chini, kama nzi. Wakianzisha mapinduzi, wazungu na watu weusi watapigana tena, na kufa kama nzi. Basi mtapata nini wakati yote yamekwisha? Rundo la maiti.

145 "Lakini paliinuka farao asiyemjua Yusufu." Ni jambo lile lile siku hizi, mtu mmoja ameinuka na akaapishwa katika—katika Ikulu, ambaye hataapa kwa kiapo chake, hatakula kiapo chake ya kwamba anaamini katika uhuru wa dini.

146 Huyu papa mpya anasema nini? Moja . . . Ana mambo manne. Moja la hayo, ni kuwaunganisha Waprotestanti na Wakatoliki pamoja. Na kwa mtu yeyote mwenye akili, hilo ndilo jambo la kufanya. Lakini kulingana na Biblia, ni vibaya kufanya hivyo. Na Biblia ilisema wangefanya hivyo.

147 Hebu twende mbele kidogo. Kwenye wakati huu, Ramesesi, huko Misri, alikuwa akikua. Nguvu zake zinakua. Mtu wa kawaida, Ramesesi, alikuwa akikua.

148 Mtu wa kawaida, yule mpinga Kristo, anakua sasa. Kupitia siasa, tayari ameingia kwenye Ikulu. Katika dini, amewakanganya sana watu wote, hata kwa kweli watashawishika na jambo hilo. Na viongozi wa kimadhehebu, karibu kila kanisa lililoko humu nchini, tayari limo katika muungano huo wa makanisa. Ramesesi anakua. Na wote wanaungana pamoja, na huo ndio watakaokuwa nao. Nao unafanya nini? Unaunda mamlaka, mnyama kama yule wa kwanza.

149 Halafu kuna mateso yatakayokuja kwa wote ambao hawatajiunga nao, na kususiwa. Itakuwa mtu umechelewa sana wakati huo. Tayari umechukua ile alama. Usiseme, "Nitafanya hivyo wakati huo." Ni heri ulifanye sasa. Ramesesi alikuwa akikua.

150 Lakini kumbuka, wakati Ramesesi alipokuwa akikua katika mamlaka, huko Misri, Mungu alikuwa na Musa nyikani. Alikuwa akikua, pia. Ramesesi alikuwa na mfumo wa kisiasa. Mungu alikuwa na mfumo wa kiroho, chini ya nabii, tayari kushuka, kunena na hao watu.

151 Wote wawili wanakua tena. Itakuwa ni shindano la kuamua, moja ya siku hizi. Wakati hauko mbali sana wakati shindano la kuamua litakapokuja. Kama ambavyo ya kawaida . . . Kama Maandiko yasemavyo, "Ya kawaida yalikuwa ni mfano wa ya kiroho." Huwezi kuliepuka jambo hilo. Hilo hapo. Liko moja kwa moja mbele ya macho yako. Ni Kweli. Hebu liangalie Kanisa sasa, likiwaita watoke, likiingia mamlakani. Roho Mtakatifu

akishuka, siri za Mungu zikifunuliwa na kuwekwa katika utaratibu. Unaona? Na papa hapa, yeye tayari yuko kwenye Ikulu. Nalo kanisa linajikusanya pamoja, amina, sio dhehebu; kutoka katika kifungo cha maovu, mbali na Waamori, watu walio huru. Loo!

152 Mungu alikuwa na Musa, atakayekuwa nabii wake. Ingawa tayari alikuwa ametabiri, na ikathibitika ya kwamba alikuwa wa kweli, bali hata hivyo alikuwa katika shule ya nyikani, amefichwa mbali na walimwengu wote. Lakini alikuwa amefunzwa, akizoezwa, huko nyikani.

153 Maadui watapendekeza, daima, mfumo wake. Na kutokuamini kutaukubali, kwa sababu adui ni ishara ya kiakili.

154 Sasa, kumbukeni, kuna wawili tu. Msisahau jambo hili. Kuna mamlaka mbili tu. Moja ni nguvu za kiroho, za Roho Mtakatifu. Hiyo nyingine ni ibilisi, akitenda kazi kwa nguvu za kielimu. Kwa kuwa, hapo ndipo alipoingilia, katika bustani ya Edeni, kupitia nguvu za kielimu, kumfanya Hawa aamini katika dhana ya kielimu, dhidi ya Neno. Ni dhahiri tu liwezavyo kuwa, watoto wangeweza kulipata hilo. Unaona? Unaona? Na hivyo ndivyo imekuwa, kote kote.

155 Hii hapa, kule Misri, asubuhi ya leo. Kuna nguvu za kielimu zinazofanya kazi kupitia kwa Ramesesi, kumleta mamlakani. Na kumwinua, ambaye hajui uhuru wa kuachilia yale Yusufu aliyokuwa amefanya, yale kanisa liliyokuwa limefanya hapo mwanzo.

156 Na sasa tunaona jambo lile lile, nguvu za kiakili zikijipenyeza miongoni mwa makanisa, nazo zimeinuliwa kufikia kwenye kiongozi wa kikanisa ambaye hajali yale Biblia iliyosema. Wana mfumo wao wenyewe. Si yale Biblia iliyosema. Ni yale kanisa liliyosema. Nao Waprotestanti wakajipenyeza moja kwa moja ndani ya jambo hilo, mpaka makundi yao yote madogo, kama hili, "Vema, hakika. Vema, ninajua inasema *Hivi*, bali nakwambia, siku hizo zimepita."

157 "Mfano wa utauwa, na wakikana nguvu zake." Kila Andiko katika Biblia linaelekeza kwake.

158 Sasa mnaona ni kwa nini ninataka kurekodi hili kwenye kanda na kuwatumia watu. Wakati umewadia. Kweli haina budi kujulikana. Kule kutoka kumewadia. Unaona?

159 Se—sehemu ya kielimu inaonekana ni kamilifu. Na ni kamilifu, ni barabara; lakini, ni uvuvio mkamilifu, wa Shetani.

160 Na halafu, wakati huo wote, ambapo, Ramesesi huyu wa kielimu alikuwa anakua na kuja kwenye kiti cha enzi. Pia kumbukeni, alilelewa kama ndugu yake Musa, unaona, ndugu yake Musa. Mmoja wao ilimbidi kuchukua kiti cha kiakili, kama tu Yusufu kwa nduguze. Nao walifanya nini na maskini Yusufu? Walimfukuza kutoka kwenye Neno. Neno ni Mungu.

Nao waliliondosha Neno, na kukubali kanuni ya imani. Na sasa kanuni ya imani imekuja mamlakani.

161 Ee Mungu, wajalie watu waone jambo hilo! Ninawezaje kutumia sauti zaidi? Ninawezaje kuifanya dhahiri zaidi kwa Maandiko, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu, kwamba tupo hapa?

162 "Loo," mnasema, "vema, sasa, kama hilo lilitoka kwa Papa Yohana, ama Papa *Nanii*, ama Askofu *Nanii*!"

Je! unaona ya kwamba Mungu alimchukua maskini mwenyeji wa nyikani asiye na sifa zozote?

Unasema, "Yote yanawezaje kuwa ni makosa?"

163 Mungu hushughulika na mtu binafsi, sio na makundi. Na mtu binafsi; Mungu akimchukua Wake—Wake, akimchukua Wake. Kitu tu alichopaswa kuwa nacho ni mtu mmoja ambaye angeweza kutenda kazi naye. Hilo ndilo tu analohitaji ni mtu mmoja. Amejaribu kuwapata, katika kila wakati. Laiti angaliweza kumpata mtu mmoja! Yeye alimpata mtu mmoja katika siku za Nuhu! Mtu mmoja katika siku za Eliya! Mtu mmoja katika siku za Yohana Mbatizaji. Mtu mmoja peke yake ndiye tu anayemhitaji. Katika siku za waamuzi, Yeye alijaribu kumpata mtu mmoja, Samsoni, akampa nguvu nyingi, bali yeye aliziuza kwa mwanamke kisha akapofushwa. Ni waamuzi; haikuwa hivyo. Mungu ndiye Mwamuzi. Unaona?

164 Unaona, leo hii, Yeye anajaribu kumpata mtu mmoja anayeweza kumshika kwa mkono Wake, ambaye atasema Kweli, ambaye hataogopa akiwa nalo, ambaye hatapatana, ambaye hatakuwa wa kulazimisha anayoamini; mtu mmoja ambaye Yeye anaweza kumshika katika mkono Wake na kulionyesha Neno Lake liko hai, na kujionyesha Mwenyewe yuko hai. Ninaamini angeweza kumpata mtu kama huyo akiwa tayari. Ninaamini. Ninaliamini. Mimi ni ninii tu . . . ninaiamini Biblia vya kutosha, kuamini ya kwamba angeweza kumpata, hiyo ni kweli, ambaye angesema Kweli.

165 Baada ya kitambo, tunaona ya kwamba, baada ya kupitia kwenye shule hizi zote. Sasa angalia. Adui anapendekeza jambo fulani, mtu wa kielimu, kwa sababu adui anatenda kazi kwenye akili. Naye mwenye elimu ataketi na kulihoji, na kusema, "Sasa, ngoja kidogo. Si ni kweli, ya kwamba halmashauri . . . "

166 Nilizungumza na mtu fulani hivi majuzi, naye akasema, "Angalia, Billy!" Yeye anafanya kazi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma, mtu mzuri. Naye akasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Wewe ni Muairishi."

Nikasema, "Naam, bwana." Kasema, "Kwa namna fulani ninalionea aibu, lakini, hata hivyo, ndivyo nilivyo."

167 Naye akasema, "Vema," akasema, "hivi hujui ya kwamba kweli, hakika, unapaswa kuwa Mkatoliki?"

168 Nikasema, "Mimi ni, en-he, ni mkatoliki wa asili, en-he." Unajua, Kanisa la kwanza lilikuwa ni Kanisa katoliki.

169 Mnaona mahali limefikia, siku hizi? Lilianza pale Pentekoste, bali dhehebu limeliweka mahali lilipo sasa. Angalieni, na Pentekoste ikarudi moja kwa moja na kujiundia dhehebu, likafanya jambo lile kanisa Katoliki la kwanza. Nao wako mbali sana leo hii kama wao walivyo, kama vile wamekuwa katika miaka elfu mbili. Na miaka hamsini imewafikisha karibu na hapo. Unaona?

170 Akasema, "Hivi huamini wakati kundi lenye elimu nyingi la baraza la ekumenia," haya basi, "linapoketi pamoja na kujadili jambo fulani, nalo kundi hilo lote linaweza kukubali, hivi hudhani watakuwa tu kidogo . . . Maana, mimi huja kukusikiliza ukihubiri," kasema, "bali sikubaliani na wewe."

171 Nikasema, "Njia pekee unayoweza kuthibitisha ya kwamba kutokubali kwako ni kwa kweli, ni kulithibitisha kwa Biblia."

Akasema, "Biblia haina uhusiano wowote nalo."

172 Nikasema, "Kwako, huenda isiwe. Lakini, kwangu mimi, Inahusika kwa yote. Unaona, Hilo ni Neno."

173 Naye akasema, "Hivi hudhani kundi la watu wenye akili ya kiekumeni likiketi pamoja, lingeweza kuwa sahihi zaidi, na liwe na uhakika wa kuwa sahihi, kuliko maskini jamaa mmoja mdogo, asiye na elimu kama wewe?" Nikasema . . . "Vema," kasema, "una shughuli gani kusema lolote dhidi ya hiyo bi- . . . ama dhidi ya kanisa le—letu? Wakati, kumekuwako na, kote katika wakati, wakati walipokuwa na halmashauri ya kwanza ya kanisa, kama ulivyolizungumzia, pale usiku mmoja, tulisikia jambo hili, nyakati za kanisa, juu ya baraza la ekumeni likikutana huko Nikea, Roma, na kuunda kanisa Katoliki la Kirumi." Kasema, "Hivi hujui kulikuwako na maelfu ya watu, wa kiroho, watu waliotumwa na Mungu walioketi kwenye baraza hilo? Pia je! hujui ya kwamba akili zao zingeweza zaidi kujua mapenzi ya Mungu, kuliko yako huku chini, baada ya Mungu kuthibitisha kwa miaka elfu mbili ya kwamba kanisa hilo ni sahihi?"

174 Nikasema, "Hajawahi kuthibitisha jambo hilo." Nikasema, "Kama kanisa hilo ni Kanisa la Mungu, hebu na tulione likizaa kama lile Kanisa la kwanza lilivyofanya basi. Hebu na tulione likifanya mambo waliyofanya mara ya kwanza. Wakati, hata Biblia inasema, ya kwamba, 'Hata hakuna nukta moja wala yodi itakayoshindwa kutoka Kwake.' Na Yeye alisema, 'Kila atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hiki, ama kuongeza neno moja Kwake, ataondolewa sehemu yake,' kama ni baraza la ekumeni ama yeyote yule, 'kutoka katika Kitabu cha Uzima.' Yeye amekwisha."

Kasema, "Billy, wewe ni mpotovu kabisa."

175 Nami nikasema, "Basi, nasadiki, wakati mmoja katika ule ukuu wa Israeli, wakati walipokuwa wametengana kama ilivyo Waprotestanti na Wakatoliki walivyofanya siku hizi, Israeli ilitaka kubaki ni Israeli." Lakini nikasema, "Tunaona ya kwamba walikuwa na mfalme jina lake Yehoshafati, mtu mwenye haki aliyejaribu kuzitii a—a—amri za Mungu. Lakini walikuwa na mwingine upande huu jina lake Ahabu, ambaye alioa mwanamke, siasa, akijaribu kufanya urafiki na taifa lingine, na akaoa mmoja wa binti zao, Yezebeli, na akamwingiza ndani, pia, miongoni mwa watu wa Mungu." Tunafanya jambo lile lile, na kuwaingiza. "Naye akawa mtawala; kumfanya Ahabu aseme *hivi*, na kumfanya Ahabu aseme *vile*." Jambo lile lile wanalofanya siku hizi. Ndipo nikasema, "Shindano la kuamua likaja."

176 Walitaka kuyaunganisha makanisa yote mawili pamoja, kama wanavyojaribu kufanya sasa. Na—na kwa Ahabu. . .Na hata Yehoshafati, mtu huyo wa kimadhehebu, alisema, "Naam. Hilo litakuwa ni sawa. Watu wako ni watu wangu. Sisi sote ni Wakristo. Sisi sote ni waaminio. Hebu na tuungane pamoja." Lakini wakati alipofikia kwenye shindano la kuamua, alisema, "Hivi hudhani inatupasa kuingia katika maombi kwa ajili ya jambo hili? Inatupasa kumtaka Bwana shauri."

Naye akasema, "Naam," Ahabu akasema.

Kwa hiyo akasema, "Hebu nikwambie. Hebu na tumtafute nabii wa Bwana."

177 Lakini, unaona, Ahabu alikuwa na mfumo aliodhani ulikuwa ni wa Bwana. Akasema, "Nina mia nne wa hao, walioelimishwa na kufundishwa." Nao wanadai kwamba ni manabii wa Kiebrania, kama vile makundi ya wahudumu yanavyodhani siku hizi.

178 Ndipo wakawatoa waje, kisha wakawauliza swali kuhusu ma—matokeo ya vita. Na kila mmoja wao akakusanyika na kuungana, kama tu baraza la ekumeni linavyofanya siku hizi, nao wakaja na swali. "Kwea. Bwana yu pamoja nawe, kwa maana nchi hiyo kweli ni mali yetu. Na uwasukume Waashuri watoke kule, ama Wafilisti. Wasukume watoke, kwa kuwa nchi hiyo ni mali yetu." Hilo linasikika ni jambo la maana sana. Unaona?

179 Lakini, hata hivyo, ndani ya moyo wa Yehoshafati, halikusikika sahihi. Akasema, "Ninajua una wahudumu mia nne wa ekumeni waliofunzwa vizuri pale. Na wote wako katika moyo mmoja, hata kufikia ambapo walifanya jozi ya pembe za chuma na kusema, 'BWANA ASEMA HIVI.' Lakini je! tungeweza kumpata mwingine mmoja tu?"

180 Akasema, "Mfalme asiseme hivyo," huyo mwanasiasa alisema. "Mfalme asiseme hivyo, kwa sababu watu hawa ni watu waliofunzwa. Nimewafunza, mimi mwenyewe." Jambo

ndilo hilo. Unaona? Jambo ndilo hilo. "Nimewafunza watu hawa. Lakini, kuna mmoja zaidi, bali ninamchukia." Unaona? Kasema, "Huyo ni Mikaya, mwana wa Imla, lakini," kasema, "Ninamchukia. Yeye si kitu ila ni mwasi kati yao. Daima anawakemea. Daima ananiambia ya kwamba nimekosea. Angalia ufalme wangu." Naam, uangalie, angalia jinsi ulivyokuwa katika machafuko.

181 Angalia dhehebu lako, siku hizi, "Lenye mfano wa utauwa bali likikana nguvu zake." Unaona? Loo, huenda mkawa na milioni moja zaidi, na elfu moja zaidi, na watu waliofunzwa vizuri zaidi, lakini mko wapi katika Roho? Nguvu zenu ziko wapi, zilizokuwa katika Samsoni, wakati aliposimama pale, kama nilvyosema hivi majuzi? Akiwa na mwili wake mkubwa pale, na kila umbile mle ndani, bali hamna Uhai ndani yake. Roho alikuwa amemwacha. Alikuwa hoi. Akiongozwa na mtoto mdogo; macho yaliyopofushwa, kwa sababu ya mwanamke fulani. Kama vile tu kanisa lilivyo, leo, likiongozwa na siasa, maaskofu, wazee, na upuuzi wa kila namna. Wanaume wakivuta majani makavu, wapate kitu kwenye kofia yao, na chochote kile. Tuko wapi? Kwa hiyo tunapofikia mahali hapa . . .

182 Wakatuma na wakampata Imla, ama nanii . . . sio Imla; bali Mikaya, mwana wa Imla. Walituma wakampata. Naye akatabiri na kuwaambia ya kwamba Ahabu atauawa kama akikwea kwenda kule.

183 Na yule askofu mkuu akampiga kofi mdomoni. Alikuwa ni mwaminifu kwa jambo hilo. Akasema, "Roho wa Mungu alienda wapi alipoondoka kwangu?"

Kasema, "Utaona." A-ha. A-ha.

184 Kasema, "Mtieni gerezani. Mtieni kwenye gereza la ndani. Mkamlishe kwa chakula cha shida, na maji ya shida. Na nitakaporudi katika amani," kasema, "jamaa huyu atanitambua."

185 Na, Imla, akijua ya kwamba alikuwa sawa na Mungu! Kwa nini? Ono lake lililingana na Neno. Yeye alikuwa ni nabii. Na roho yake na ono lake vililingana kabisa na nabii, Eliya. Akasema, "Ukirudi, kamwe, basi Mungu hakuwa amesema na mimi."

186 Sasa, nilimwambia jamaa huyu, "Ni nani aliyekuwa sahihi, hilo baraza la ekumeni ambapo watu mia nne waliketi pamoja, waliochaguliwa na wanadamu, ama maskini huyo mwasi aliyechaguliwa na Mungu?"

"Vema," akasema, "vema, ungejuaje tofauti yake?"

187 Nikasema, "Rudi kwenye ile Ramani!" Tunajuaje kujenga jengo pasipokuwapo na ramani?

188 Kama wangalisimama kwa dakika moja, na kuona ya kwamba yule nabii, Eliya, alimlaani Ahabu, na kusema, "Mbwa

watairamba damu yake." Na waliiramba. Yeye angewezaje kubariki kile Mungu alichokuwa amekilaani?

189 Unawezaje kubariki kitu chochote ambacho Mungu amekilaani? Tokeni kwenye kitu hicho. Ondokeni kwake. Njoni ndani ya Kristo. Amina.

190 Sasa angalia. Lakini, adui atapendekeza. Adui atakusudia jambo fulani, aliandae, nao watu wenye bongo watasema, "Hiyo ni kweli."

191 Hapo ndipo huyu ndugu wa thamani alipokuwa. Mtu huyu, alisema, "Yaonekana kana kwamba . . . Angalia hapa. Unajua, ya kwamba, kama sisi sote tungekuwa pamoja, kama kanisa moja, hivi huoni tungekuwa bora zaidi kuliko tulivyotawanyika sasa?"

192 Hilo si linasikika ni zuri, kama Waprotestanti wote na Wakatoliki wangeweza kukusanyika pamoja na kufikia mapatano fulani ya pamoja? "Lakini watu wawili wanawezaje kutembea wasipokuwa wamepatana?" Mnawezaje, wakati kundi moja *hapa* haliamini katika uponyaji, hilo *lingine* linasema kweli wanauamini, hilo *lingine* linauweka kwenye wakati mwingine huko nyuma? Wengine hata hawaiamini Biblia. Na ukiyaweka hayo pamoja, una nini? Mungu siye mwanzilishi wa machafuko.

193 Kabla ya Mungu kuliweka Kanisa Lake katika utaratibu, walingojea siku kumi usiku na mchana, mpaka wote wakawa "mahali pamoja, katika umoja." Ndipo akaja Roho Mtakatifu kwa ajili ya uongozi, sio baraza fulani la ekumeni. Unaona? Ninatumaini mnalipata hili. Angalieni.

194 Huyo ni asiyeamini, asiyelitii Neno la Mungu, ambaye haoni vile Neno linavyosema, bali unaona hoja zako mwenyewe. Hivyo ndivyo Hawa alivyofanya, kwanza kabisa. Alitegemea hoja zake.

195 Shetani akasema, "Sasa, angalia hapa. Hivi si ni jambo la maana? Ninajua Neno linasema *Hivyo*. Lakini, ngoja kidogo, hivi si ni jambo la maana kwamba—kwamba ungekuwa bora zaidi kama ulijua mema na mabaya?"

"Naam, kweli." Ndipo akalila. Hakika.

196 Hivyo ndivyo ilivyo na hoja. Sasa, kutokuamini daima kutaanza kutoa hoja nyingi, bali imani haitaligusa jambo hilo.

197 Hivi si ingekuwa ni jambo la maana kwa baba yetu; ambaye ni baba wa imani yetu, Ibrahimu, kwamba sisi ni watoto wake kwa "kuwa ndani ya Kristo." Hivi si ingekuwa ni wazi kwamba mwanamke mwenye umri wa miaka sitini na mitano, na alikuwa ameishi pamoja naye, tangu alipokuwa msichana, asingeweza kupata mtoto? Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, ama tisini, naye mia moja, na wangali hawana mtoto. Hivi si ingekuwa vizuri, kundi kubwa la madaktari na sayansi kumfanyia Sara uchunguzi? Kasema, "Mbona, tumbo lake la uzazi limekauka. Mishipa ya maziwa imekauka, miaka arobaini

iliyopita. Moyo wake, kwenye umri huo, asingeweza kuingia katika utungu wa kuzaa." Mbona, ni hoja tu.

198 Lakini Ibrahimu alikataa jambo hilo. "Hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini. Dhidi ya hoja, hakusita katika ahadi ya Mungu, haidhuru ilikuwa ni nini. Kwa kuwa yeye—yeye alikuwa ameamini kwamba Mungu anaweza kufanya kila kitu ambacho alisema angefanya."

199 Sasa, wako wapi wana wa Ibrahimu asubuhi ya leo? Ninyi wahudumu mnaoogopa, mnahofu, juu ya chakula chenu na maji, mtaani, kama mkiondoka kwenye hiyo Babeli. Imani yenu iko wapi? Daudi alisema, "Wakati mmoja nalikuwa kijana, nami sasa ni mzee. Sijamwona mwenye haki ameachwa, wala Mzao Wake akiomba chakula." Msiogope. Dumuni waaminifu kwa Kristo.

200 Lakini kutokuamini kutaingiza hoja. Hivyo ndivyo kulivyofanya. Sasa mnalipata? Kutokuamini kunategemea hoja, mambo ya siku hizi. Imani haitafanya jambo hilo.

201 Imani huliangalia Neno. Bali imani hujiweka kwenye Mwamba usiotikisika, Neno la Milele la Mungu. Amina. Imani haiangalii hoja. Sijali ni kiasi gani unavyoweza kuonyesha ingekuwa ni bora zaidi. Kama Neno linasema "la," imani hutulia hapo. Hiyo ndiyo madhabahu ya mahali pa kupumzikia pa imani.

202 Ninataka kuwaulizeni ninyi Walutheri, asubuhi ya leo, ninyi Wabaptisti, na ninyi Wakatoliki, na ninyi, chochote mlicho, ninyi watu wa kimadhehebu kote ulimwenguni. Mnawezaje kuiweka imani yenu katika dhehebu lenu, wakati ni kinyume na Neno? Hivi mna imani ya aina gani? Mna nguvu za kuhoji, wala sio imani. "Kwa maana imani chanzo chake ni kusikia," kulisikiliza baraza la ekumeni? Je! ungeweza . . . Kasema, ungeweza kupata hilo katika Shajara ya Mwaka ya Siku ya Kuzaliwa Kwa Mama Wakongwe, bali kamwe hulipati katika Neno la Mungu.

203 "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia kwa Neno la Mungu." Amina. Niambie kwamba mtu mmoja anaweza kusema lolote kinyume na Hilo, na kusema eti ni Neno la Mungu. Wakati, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitapita."

204 Imani hulifanya Neno madhabahu yake ya kupumzikia. Inajongea moja kwa moja hadi juu ya ule Mwamba wa Milele, Kristo Yesu, lile Neno, na kukaa pale na kupumzika. Acha upepo uvume vikali. Acha tufani itikise. Iko salama, milele. Inapumzika pale pale kwenye Neno hilo. Hapo ndipo imani, imani halisi ya Kikristo, inapostarehe. Mahali pa kupumzikia ni Neno, kwa kuwa inajua ya kwamba daima Mungu atathibitisha ya kwamba Yeye ni mkuu zaidi, juu ya kila mmoja wa adui Zake. Haidhuru linaonekana ni jambo baya jinsi gani, na jinsi ambavyo adui ameingia, na jinsi inavyoonekana kana kwamba umeshindwa, imani ingali inajua.

205 Sasa, kwenu ninyi watu wagonjwa, loo, jinsi ningalitaka kutilia hili mkazo kabisa! Unapoishika imani hiyo, kwamba utaponywa; kila—kila hali ya mambo, kila kitu, ishara zote, dalili zote zinaweza kuonyesha ya kwamba wewe unakufa, kamwe hutasogea! Mahali pake pa kupumzikia ni kwenye madhabahu ya Neno la Mungu, wakati imani, imani halisi inapojiweka hapo. Si kujifanya kuamini sasa; imani. Sio tumaini; bali imani. Tumaini liko *hapa* nje, likitumaini ya kwamba lilikuwa liko ndani. Imani iko ndani tayari, ikiangalia nje, na kusema, "Imetendeka." Unaona? Hiyo ndiyo imani. Hapo ndipo imani inapochukua mahali pake pa kupumzikia, kwa maana inajua ya kwamba Mungu kamwe, kamwe hatamwacha adui apae juu Yake. Hajamwacha kamwe. Imani inajua hilo, kwa hiyo, haidhuru jambo hilo lilionekanaje.

Nuhu alijua ya kwamba ile safina ingeelea. Unaona? Hakika alijua.

Danieli alijua ya kwamba Mungu angeweza kukifunga kinywa cha simba.

Wana wa Kiebrania walijua ya kwamba Mungu angeweza kuuzima ule moto.

206 Yesu alijua ya kwamba Mungu angemfufua tena, kwa sababu Neno lilisema, "Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Yeye alijua uharibifu ungeingia katika saa sabini na mbili. Akasema, "Katika siku tatu nitafufuka tena." Unaona? Ilichukua mahali pake pa kupumzikia Milele katika madhabahu ya Neno la Mungu, na ikasimama hapo.

207 Hoja itajaribu iwezavyo kutambua, "Vema, hapana shaka mfumo *huu* ni bora zaidi. *Huu* ndio Ule." Unaonekana ni bora zaidi kwa kuwa unaangalia kwa nia ya kielimu. Unaweza kuthibitisha hoja.

208 Bali huwezi kuithibitisha imani. Maana, kama unaweza kuithibitisha, si imani tena. Ila imani inajua tu Neno na ahadi, nayo inakiangalia kile kitu ambacho hukioni. "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Huwezi kutoa hoja. Siwezi kuthibitisha jinsi litakavyofanyika. Sijui jinsi itakavyofanywa. Sijui, bali ninaamini. Ninajua kwamba ndivyo ilivyo, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.

209 Hiyo ndiyo sababu ninajua ya kwamba Hili ni kweli. Ninajua Neno ni la kweli. Ninajua Ujumbe ni wa kweli, kwa kuwa umo katika Neno. Nami ninamwona Mungu aliye hai akitenda kazi miongoni Mwake, kuthibitisha. Tuko katika kutoka, kweli kabisa.

210 Hata mauti yenyewe haiwezi kuitikisa imani. Watu wanasimama tu moja kwa moja katika mauti, katika ninii . . . moja kwa moja mbele ya mauti, na kuushangilia ushindi wa

ufufuo. Paulo, "Ewe mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, ku wapi kushinda kwako?" Unaona? "Maana, Kristo alifufuka, na hao walio katika Kristo watafufuka pamoja Naye katika kule Kuja Kwake." Unaona? Haiwezi kuibadilisha. Naam.

211 Imani hulifanya Neno la Mungu madhabahu yake ya raha yake ya Milele. Inakaa kwenye Neno la Mungu. Angalieni, tena.

212 Sasa, tuna muda kidogo tu zaidi, kama dakika ishirini na tano, kama ninyi—kama hamjali. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na—nataka kuiendeleza kanda hii, kidogo tu.

213 Hebu mwangalieni yule mfalme, yule mfalme mpya ambaye aliinuka, ambaye hakumjua Yusufu. Njama yake ya kwanza ilikuwa ni nini, kuziangamiza nguvu za Israeli? Ilikuwa kwa watoto wao. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye alijaribu kuwaangamiza watoto wao. Sasa sikilizeni kwa makini. Ibilisi yeye yule, katika umbo tofauti la utawala, alijaribu kumwangamiza Mwana wa pekee wa Mungu. Unaona? "Waangamize hao watoto, kwanza, kabla hawajapata msingi." Ibilisi kweli ni ndege mwerevu sana, mjanja. Anajua jinsi ya kupiga kitu hicho kabla hakijaanza. Anajua jambo hilo. Unaona?

214 Na jambo pekee unaloweza kufanya, kumshinda, ni kumtegemea Kristo, na kujinyenyekeza na kumwacha akuongoze. Unaona? Kamwe hutaweza kufanya jambo hilo vinginevyo. Nguvu zako za kiakili hazitalifanya. Inakubidi kuamini. Mtegemee tu Yeye. Yeye ndiye Mchungaji. Si kazi ya kondoo kumfukuza mbwamwitu. Ni kazi ya mchungaji. Lakini kondoo hana budi kukaa pamoja na mchungaji, kusudi akae salama. Hiyo ndiyo zoni yangu ya usalama, ni katika Kristo; na Kristo ni Neno. Hiyo ndiyo zoni ya usalama.

215 Angalia. Ibilisi, katika umbo la—la Ramesesi, mfalme, jambo la kwanza alilofanya ni kuwaangamiza watoto, kwa mauti ya kawaida. Na mara Mwana wa Mungu alipozaliwa . . . Alikuwa ametoka Misri, maana Mungu aliangamiza Misri, aliilaani. Haijapata kuinuka tena asilani, tangu wakati huo. Kisha akawa huko Rumi; Shetani alihamisha kiti cha—chake akakipeleka Rumi. Na jambo la kwanza Rumi ilichofanya, kuwaangamiza wote, kumpata, kuwa na hakika; ibilisi, katika mfumo huo wa Kirumi, alijaribu kumwangamiza (nani?) Mwana wa Mungu, kwanza. Ibilisi yeye yule!

216 Na, leo hii, amefanya jambo lile lile, chini ya ishara ya roho sasa, ya kidini, inayokiri Ukristo, na kuwachukua wasichana wetu na kuwaoza kwa wavulana Wakatoliki, na kuwafanya wawalee watoto wao Kikatoliki, kuvunja nguvu za upande huo mwingine. Huyo hapo pepo wako. Huyo hapo shetani wako ameketi juu ya vilima saba, amevaa taji yenye sehemu tatu, mwenye hila na mjanja sana, mwerevu, mwenye elimu kama yule

nyoka; uzao wa nyoka, watoto wake, wakitumia mbinu zile zile za kiakili. Angalieni.

217 Kisha wakawaua watoto, katika nyakati zile zingine mbili. Waliwaua watoto kwa kitu gani? Mara mbili. Sasa kumbukeni, angalieni hizo mbili, na hizo tatu. Unaona? Yeye aliwaua watoto, mara hizo mbili za kwanza, kwa mauti ya kimwili. Na wakati huu wa mwisho, yeye anawachukua watoto hao na kuwaua kwa mauti ya kiroho, wakioa, wakioana.

218 Hivi Danieli hakusema jambo lile lile, katika ufalme huu wa chuma na udongo, ya kwamba watazichanganya mbegu hizo, wakijaribu kuvunja nguvu za hao watu wengine? Na hivyo ndivyo wanavyofanya, mpaka wamekichukua kitu hicho sasa. Wamemwingiza rais. Sasa, jambo lingine linalokupasa kufanya, ni kumwingiza—ni kumwingiza kadinali. Kuweka baraza lote la mawaziri mle ndani, ndipo mtafanya nini?

219 Jambo lifuatalo watakalofanya, watazichukua fedha zao na—na kulipa deni ya Marekani, na waikope kutoka kanisani, ndipo basi mmekwisha kuuzwa. Sasa, siku hizi tunanii—tunaishi, tunayalipia madeni yetu ya kigeni kule, kwa fedha za kodi ambazo hazitalipiwa mpaka miaka arobaini itakapopita. Hatuna fedha tena. Bali kanisa linazo. Hivi Biblia haisemi, "Alikuwa amepambwa kwa dhahabu"? Na, loo, jamani! Lakini ninyi . . .

220 Hivyo ndivyo linavyofanya, mnaona, kuwaoza binti zenu, mabinti wanaolewa na wana wenu, wanawalea watoto wenu Wakatoliki, kweli kabisa, linawaua kwa mauti ya kiroho. Hivi Biblia haikusema, ya kwamba, "angemtupa katika kitanda cha mambo ya ulimwengu, na kuwaua watoto wake kwa mauti ya kiroho"? Ufunuo 17. Unaona?

221 Daima ni Neno. Sijali unaenda wapi, bado ni Neno. Halina budi kuenea moja kwa moja katika picha. Kama halienei, silo Neno, silo Neno. Usipoweza kulifanya liende moja kwa moja kote katika Biblia, basi si la kweli.

222 Angalia. Kwenye wakati huu, Mungu alikuwa akimfundisha mtumishi Wake kwa ajili ya kazi yake. Akimfundisha, mbali nao, mbali na mipango yao, njama zao. Mnalipata? Nje ya mfumo wao wa kimadhehebu, Mungu alikuwa akimfundisha mtu kwa ajili ya kusudi Lake. Aliziachilia tu ziendelee. Akamwacha aoe, na awe na mkewe na watoto, mtoto Gershomu. Alikuwa akiishi maisha mazuri kweli, akimbariki huko nje. Lakini, wakati wote, Yeye alikuwa akimwandaa, akimfundisha.

223 Mungu na adui Wake walifanya, katika hali ya kawaida wakati huo, kama tu vile Mungu na adui Wake wanavyofanya katika hali ya kiroho sasa. Waliwaua kwa mauti ya kimwili; sasa kwa mauti ya kiroho. Unaona? Mungu alikuwa akimwandaa mtu wa kawaida, nabii Wake, ashuke kwenda Misri. Na Shetani alikuwa akimwandaa Ramesesi, mtu wake wa mwilini,

unaona, akimwandaa mtu wa mwilini (akafanye nini?) akaue, ama akawaunganishe Wamisri wote na Waebrania pamoja, na kuwafanya waendelee kuwatumikia.

224 Hiyo ndiyo sababu ni vigumu sana kwa akili kutoa hoja dhidi ya mfumo wa elimu unaoweza kuthibitisha pointi zake. Unaona? Hiyo ni kweli. Moyo wake daima utaelekea kwenye elimu. Watu wenye akili na wenye kuhoji hata hawalioni.

225 Je! mliangalia ile *Amri Kumi* ya Cecil DeMille? Nadhani wengi wenu mliiangalia. Siamini katika kwenda kwenye sinema, upuuzi huu wote. Bali nilipendekeza kwa kanisa, ya kwamba mtu yeyote, kama hawakuwa na chochote ila hiyo, waliotaka kuiangalia, ingekuwa ni sawa kama wanataka kuiangalia. Kwa sababu, nisingeruhusu . . . Kwanza, baadhi ya ndugu zangu walienda. Walikuja, wakaniambia. Sijapata kuangalia moja kwa miaka mingi. Hatimaye, nilishuka nikaenda hapa chini, wakati ilipokuwa kwenye uwanja huu wa sinema. Nikaiangalia. Nikaona kile ilicho. Ndipo nikaliambia kanisa, "Mkitaka kwenda kuiona hiyo, ni sawa." Hiyo hapo. Ilikuwa ni nzuri sana, ya kupendeza.

226 Jinsi ambavyo ile mbinu ya ibilisi, jinsi alivyokuwa mjanja mle ndani, jinsi ambavyo a—aliingia mle kuwaua watoto hao. Na jinsi ambavyo watu wenye elimu waliichukua na kuiamini, kwa kuwa wangeweza kuiona! Ilikuwa ni ya maana. Loo, jinsi Mungu alivyokuwa, wakati wote, akimfundisha nabii huyu! Na jinsi ambavyo Misri ilikuwa ikimfundisha, katika siasa, huyu Ramesesi, apate kuingia mamlakani! Na ndipo yale mashindano makuu yakaja, siku moja, kati ya nguvu za kielimu na za kiroho. Na Ramesesi, pamoja na miungu yake yote, alikuwa amesimama pale na kumwaga maji ndani yake, ku—kumbariki mungu wa Nile. Mungu alimpiga, na damu ikatiririka kutoka kwake. Alikuwa . . . Loo, ni—nilidhani lilikuwa ni jambo la kushangaza sana, unaona, kuona yale yaliyotukia. Loo!

227 Sasa angalia. Mtu wa elimu daima ataanza kutoa hoja. Wala haiwezi kuona upande wa kiroho, kwa maana ni ya kielimu. Loo, wala isingeweza wakati mwingine wowote! Hawawezi kuliona sasa.

228 Wasingeweza kuliona katika siku za Eliya. Nabii huyu mmoja aliyejaa ndevu za kipilipili angewezaje . . .

Mungu na anisamehe kwa kusema jambo kama hilo. Lakini ni—ninalinganisha vibaya . . . Na Mungu anajua ya kwamba ninajaribu kulifanya—kulifanya la kukebehi niwezavyo, kusudi mpate kumwona Ro—Roho wa Mungu.

229 Kama vile Paulo alivyosema, "Kamwe sikuwajia, nikizungumza kwa maneno yenye kushawishi na ya hekima, kwa kuwa akili zenu zingevutiwa na hekima hiyo. Bali niliwajia kwa nguvu za Roho Mtakatifu, ili ninii lenu—ili lenu—lenu—tumaini

lenu na imani vitulie, sio katika hekima ya mwanadamu, bali katika nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo."

230 Hiyo ndiyo sababu ninalifanya hili la dhihaka sana, kwa kumwita yule nabii mkuu, mcha Mungu, "aliyejaa ndevu za kipilipili." Kwa sababu, huenda alikuwa anaonekana ni m—mtu mwenye hali mbaya sana, kusimama, kando ya kuhani aliyevalia nadhifu, na kujiita mtu wa Mungu.

231 Mwangalie. Ungeweza kuuona utakatifu wa kuhani huyo, kwa akili za kielimu. Ungeweza kukiona kile kilemba kichwani mwake, na ninii uliopinduliwa...na ile naivera imewekwa kifuani mwake *hapa*. Ungeweza kuona yale mafuta ya kumiminwa, ya kawaida, juu ya ndevu zake, yakitiririka hata kwenye pindo za joho lake. Ungeweza kuona mioto ya dhabihu ikiwaka, na kawaida zote za dini katika utaratibu. Sasa, hayo ndiyo watu wa kawaida wangeliyaendea.

232 Hivyo ndivyo wanavyojaribu kufanya siku hizi, jicho, lango la kuingia kwenye nafsi. Lakini, unaona, lile jicho la kiroho nyuma katika jicho hilo!

233 Walimwangalia maskini mzee huyu aliyejaa mandevu ya kipilipili amesimama pale, nywele kifuani mwake; na amejifunga kipande kikubwa mno cha ngozi ya kondoo, cha ngozi, mshipi viunoni mwake, akiwa, labda miguu mitupu, maskini mikono iliyokonda, huku nyama zimetepwereka *hivi*; na ndevu nyeupe, zimening'inia kote usoni mwake; na fimbo iliyopinda mkononi mwake, amesimama pale. Lakini jicho la kiroho lingeweza kuona nguvu za Mungu zikitenda kazi pale, maana alikuwa yuko kwenye Neno kikamilifu. Si yale akili za kielimu zinayoona; bali yale macho ya kiroho yanayoona!

234 Na—na macho ya kawaida, leo hii, huona kanisa linalovutia sana, ushirika ulio na meya wa jiji, ama—ama chochote kile, katika mashirika haya ya kimadhehebu. Nao wanashindwa kuona nguvu za Roho Mtakatifu, wakati zinapoweza kuwafufua wafu na kuwaponya wagonjwa. Na—na—na jinsi... Unaona? Hao, wanaangalia, nao wanaangalia Hollywood, na wanawaangalia watu mtaani.

235 Wanawake, siku hizi, wanafikiria, "Vema, mwanamke *huyu*, Susie, yeye ni mfuasi wa kanisa. Amezikata nywele zake. Anajipodoa. Kila mtu mjini anampenda."

236 Nashangaa kuhusu Mbinguni? Unaona? Wakati likiwa ni kinyume na Neno, Mungu hawezi kuliidhinisha. Yeye, angekuwa akiliidhinisha dhidi Yake Mwenyewe. Angekuwa akilikana Neno Lake Mwenyewe. Na ijulikane, Mungu kamwe hatafanya hivyo, hata mbingu na nchi zipite. Mwanamke aliyezikata nywele zake ni laana, machoni pa Mungu, ama mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume. Unaona? Jicho la kiroho hushika Hilo; wanaishi kwa ajili ya Mambo Yajayo. Mtu wa mwilini anaishi apate kuyatolea hoja mambo ya kimwili ya siku hizi.

237 Angalia sasa, Mungu akifanya jambo hili, na hata hivyo watu hawakulijua jambo hilo. Watu wa kimwili walikuwa wakiishi kwa hoja. Mungu sasa anaita kutoka kwa kiroho. Ambapo aliita kutoka kwa maumbile ya kawaida kwa watu Wake, Yeye anaita kutoka kwa kiroho siku hizi, kwa (akina nani Wake?) Wateule Wake, kwa Wateule Wake pekee.

238 Sasa, Misri isingeweza kuona kwamba Israeli walikuwa sahihi, ingawa damu ya mwana-kondoo ilikuwa mlangoni na kwenye kizingiti cha juu, na mambo yaliyokuwa yakitukia.

239 Na Mungu kule chini, akitenda kazi katika nabii huyu, na akichukua neno la mwanadamu. Anamwacha asimame pale, na kuchukua fi—fimbo aliyokuwa akiegemea, na kuielekeza mashariki, na akasema, "Nzi na waje, na wajae kwa uzito sana juu ya Wamisri." Akarudi pale nyuma.

Na kila mtu akasema, "Hakuna kitu kilichotukia. Hakuna kitu kilichotukia."

240 Lakini kitambo kidogo tu, nzi mchafu wa kijani kibichi hapana budi alianza kuzunguka hapo. Baada ya muda kidogo, walikuwa labda ratili mbili kwa yadi moja mraba, ambao mwanadamu alinena uumbaji ukawepo.

241 Hapo palikuwa na Ramesesi wa kielimu akiwa amesimama pale, aliyepinga; mtu wa kidini sana, na anapinga Roho wa Mungu aliye hai. Nao watu wa kimwili wangeweza tu kumwona Ramesesi. Bali mtu wa kiroho aliiona ile ahadi, na akaiona ikija kutimia.

242 Vema, kama Yoshua na Kalebu wangeweza kuwakabili hao Waamaleki, na Wahivi, na Wayebusi, kana kwamba hawakuwako, hata hivyo wakiwazidi wingi mara mbili, ama mara tatu ama mara nne. Na watu wa kimwili, pale Kadesh-barnea, wakati wale wapelelezi walipoenda huko, walisema, "Aha, hatuwezi kuwakabili. Sisi . . . Wao ni—wao wametuzidi mno. Vema, sisi ni kama—sisi ni kama nzige, mbele zao."

243 Lakini Kalebu na Yoshua waliiona ahadi ya Mungu, wakasema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuwashinda." Kwa nini? Walikuwa wakiangalia, "Mungu alisema, 'Nawapa nchi hiyo.'" Unaona? Mtu wa kimwili halipati. Mtu wa kiroho hulipata.

244 Na ni kwa nini? Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Ni kwa nini Wamisri hawakuyaona mambo haya? Ni kwa sababu hawakuwa wameteuliwa. Mungu alimwambia Ibrahimu kabla halijatukia. Lipateni, enyi kanisa linalolala! Mungu alimwambia Ibrahimu kabla halijatukia, "Uzao wako utakuwa mgeni katika—katika Misri, kwa muda wa miaka mia nne, na Mimi nitawatoa." Hiyo ndiyo sababu waliliona, kwa kuwa waliteuliwa wapate kuliona. Hao ni wateule. Israeli iliteuliwa kuiona ahadi ya Mungu, nao wakatoka Misri, ambako wasioamini waliangamia.

245 Na, leo hii, Mungu anawaita wateule Wake, Uzao wa kiroho wa Ibrahimu, kwa imani aliyokuwa nayo katika Neno la Mungu. Hivi hamwoni ule Uzao wa kiroho, leo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ambao haulioni kanisa la kimwili. Unaliona Neno. Nao unaitwa kutoka kwenye hayo madhehebu makubwa, waingie Uweponi mwa Yesu Kristo. Hilo lilikuwa dhahiri? Mlilipata? ["Amina."] Vema. Tutaenda mbele zaidi. Wateule, peke yao!

Daktari D.L.Ph., kamwe hawalioni. Hawakuteuliwa.

246 Pia, kumbukeni, uteuzi huu, unaokuja sasa, si kuenda tu kwenye taifa lingine, ni kuenda Utukufuni, ambako majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Sio chini ya maskini yule mwana-kondoo mnyama aliyewatoa Israeli, ambapo wangeweza kurudi nyuma kutoka huko na kurudi walikotoka. Lakini, hii haiwezi. Hii iko chini ya Damu ya Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na majina yao yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na yamo mle ndani, wameteuliwa. Na wakati Nuru hiyo inapomulika juu yao, namna hiyo, hizo kuta za kimadhehebu zinaporomoka na kuwaondokea, nao hawa hapa wanakuja. "Tokeni kati yao," amesema Roho Mtakatifu katika siku hizi za mwisho. "Msiguse vitu vyao vichafu. Nitakuwa Mungu kwenu; ninyi iweni wana na binti Kwangu." Sasa, angalia.

247 Israeli walikuwa wakiangalia. Walijua ya kwamba Mungu alishughulika na manabii Wake. Wao. . .Neno liliwajia, nao wakaja kuliona. Nao wakaliona.

248 Na sasa ishara ya kielimu, tunaiona sasa, kwamba wao wanaamini madhehebu yao. Wangali wamo katika kanuni zao za imani. Hata hivyo wao . . .

249 Ni kama tu Balaamu alivyokuwa, aliyekuja kwenye kilele cha kilima, mahali Israeli walipokuwa. Hao hapo Israeli, sio taifa, walikuwa ni watu tu wakielea hapa na pale, nao walikuwa na hatia. Na Moabu, ndugu yake, mwenye elimu, mtu wa madhehebu, alikuja juu ya kile kilima, pamoja na askofu ama nabii waliyekuwa naye, na akajenga madhabahu, na kutoa dhabihu ile ile. Bali alishindwa kuiona ile Nguzo ya Moto na Mwamba uliopigwa miongoni mwa Israeli.

250 Ndivyo ilivyo siku hizi. Wenye elimu walikuwa wakiangalia watu mashuhuri waliokuwa wamesimama pale. Wanashindwa kuuona Mwamba uliopigwa. Hata na askofu, mwenyewe, anashindwa kuziona nguvu za Roho Mtakatifu, makelele ya Mfalme kambini. Wanashindwa kuona hayo.

251 Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo tena siku hizi. Mungu anawaita watu Wake walioteuliwa, nao wameteuliwa sasa. Na sasa

wameteuliwa kwa sababu gani? Kwa ajili ya ufufuo. Na ni ishara ya namna gani anayowaonyesha? Ishara ya kufufuka.

252 Alikuwa akiwaonyesha nini wakati ule? Ishara ya ukombozi, kuwakomboa na utumwa, ishara ya nguvu ambazo zingeweza kuzifunga mbingu ama ambazo zingeweza kuzitia mbingu giza.

253 Na sasa anaonyesha nguvu za kufufuka kwa Mwanawe akiishi miongoni mwao, kuwafufua kutoka kwenye kaburi hili na makaburini tunamoishi, kutupeleka kwenye Nchi ambayo Yeye ametuahidia. Ishara ya Kufufuka, kuwaita kutoka Misri ya kiroho na Babeli ya kiroho, akiwa ametambua.

254 Hebu niseme jambo hili pole pole sasa, mpate kulishika. Akilifanya kwa mfumo ule ule aliofanya pale mwanzo, anafanya jambo lile lile. Anayapofusha macho ya asiyeamini; anayafungua macho ya mwaminio. Basi angalia siasa zinalifanya hilo kwenye upande wa kielimu, siasa na kanisa, siasa na mataifa, kila kitu; na upande huo mwingine umefichwa kwao, tendo la kiroho.

255 Mungu alimpeleka mtu mmoja nyikani, akamfunza. Kisha akamrudisha, na kukipeleka kitu hicho huko, kisha akawatoa hao watu. Mnaona ninalomaanisha? Yeye hawezi kubadilisha mpango Wake. Yeye ni Mungu. Kamwe hatajishughulisha na kundi. Kamwe hajafanya hivyo. Yeye humshughulikia mtu mmoja; na alifanya hivyo, na atafanya hivyo. Na aliahidi, hata katika Malaki 4, angefanya hivyo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kuna ahadi Yake, kwamba Yeye alikuwa ni nani; ahadi ya kile alichosema Yeye angekifanya, na basi tumewasili. Tunapaswa kuwa ni watu wenye furaha jinsi gani; akiwapa ishara, kwa ishara ya Neno Lake lililoahidiwa, Neno lililoahidiwa. Aliahidi angefanya hivyo. Na wao . . . "Atairudisha Imani ya hao watu, mioyo ya watu hao, ielekee Imani ya baba wa asili wa kipentekoste." Aliahidi kufanya hivyo, akionyesha ishara Zake.

256 "Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Makanisa yaliona ishara za namna gani Sodoma? Hilo kanisa la kielimu liliona kitu gani? Wahubiri wawili. Nalo Kanisa la kiroho, lililoteuliwa, Ibrahimu na kundi lake waliona nini? Liliona Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa nyama, mwili wa kibinadamu, ambao ungeweza kuitambua roho na kujua kile Sara alichokuwa akisema nyuma yake. "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Tunamwona Roho Mtakatifu miongoni mwetu, akifanya jambo lile lile, akitenda kazi katika mwili wa mwanadamu. Hii ndiyo ile saa. Unaona? Tupo hapa tu, enyi marafiki. Hivyo tu. Kutoka kunaendelea.

257 Lakini sasa angalieni, Yeye alifanya jambo hilo wakati huo kwa kitu gani? Angalieni, na mvae mawazo yenu ya kiroho. Roho Mtakatifu na aweke kando maskini kofia ya kale ya kutokujali sasa, na mwangalie kwa makini. Mungu akipata kufanya uamuzi

wa kufanya jambo lolote, kwa njia moja, Yeye kamwe hawezi kuibadilisha.

258 Katika bustani ya Edeni, wakati alipotaka kumkomboa mwanadamu arudi kwenye ushirika, Yeye alifanya uamuzi: ilikuwa ni damu. Walijaribu elimu, wamejaribu dhehebu, wamejaribu kutaifisha, na chochote kile, wala kamwe halifanikiwi. Kuna mahali pamoja pekee ambapo Mungu atakutana na mwanadamu, hapo ni chini ya damu iliyomwagika, kama ilivyokuwa katika Edeni. Halijabadilika kamwe. Mahali pekee ambapo Mungu alikutana, katika siku za Ayubu, palikuwa ni chini ya mwana-kondoo wa sadaka. Mahali pekee alipokutana katika siku za Israeli, chini ya mwana-kondoo wa sadaka; kama alivyofanya katika bustani ya Edeni, chini ya mwana-kondoo wa sadaka.

259 Mahali pekee anapokutana siku hizi, sio katika madhehebu; wanazozana na kubishana miongoni mwa mmoja kwa mwingine. Sio katika ukanisa; wangali wanafanya jambo lile lile. Sio katika wenye elimu; wote wamechanganyikiwa. Bali chini ya Damu ya Mwana-Kondoo, kila mwaminio anaweza kukutana kwa ushirika, palipo na Uzima.

260 Mungu alichagua, katika siku za kule kutoka, Yeye aliliita kundi moja litoke. Na kutoka kwenye kundi hilo, ninawataka muone jambo fulani, Yeye alipata tu wawili walioingia kwenye nchi ya ahadi. Yeye alichagua kuwatoa kwa kutumia nini, siasa, dhehebu? Yeye alichagua nabii, akiwa na ishara ya kimbinguni ya Nguzo ya Moto, watu wasije wakakosea. Yale nabii aliyosema yalikuwa ni Kweli. Na Mungu alishuka, Nguzo ya Moto, na kujithibitisha Mwenyewe, akaonyesha Neno Lake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ndiyo aliyoileta, kutoka Kwake kwa kwanza. Kutoka Kwake kwa pili . . .

261 Mungu daima huenda katika tatu. Yeye ni mkamilifu katika tatu. Ninyi nyote mmeyaona mahubiri yangu, daima ni tatu na saba. A-ha. *Saba* ni "timilifu." *Tatu* ni "ukamilifu Wake." Mvuto wa Kwanza, wa Pili, na wa Tatu. Na, loo, yote, kila kitu. Unaona? Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Kila kitu! Unaona? Angalieni.

262 Yeye alifanya nini, kule kutoka kwa kwanza? Alimtuma nabii, aliyetiwa mafuta kwa Nguzo ya Moto, naye akawaita watu wakatoka. Huko kulikuwa ni kutoka Kwake kwa kwanza.

263 Na wakati wa Israeli ulipokwisha, Yeye alimtuma tena, Mungu-Nabii, akiwa na Nguzo ya Moto. Yohana aliiona ikishuka kutoka Mbinguni kama hua. Na Yeye akasema, "Ninaenda kwa Mungu na ninarudi kwa Mungu."

264 Baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka; Sauli wa Tarso, akienda zake Dameski, aliona Nguzo ile ile ya Moto. Naye akiwa ni Mwebrania, aliyefunzwa vizuri katika Neno, alisema,

"Bwana, U nani Wewe?" Alijua ilikuwa ni Bwana, ile Nguzo ya Moto. Yeye alikuwa ni Mwebrania. Kasema, "U nani Wewe?"

Na Yeye akasema, "Mimi ni Yesu."

265 Kutoka kwa pili, Yeye alimleta Nabii, aliyetiwa mafuta, ambaye alikuwa ni Mwanawe, Mungu-Nabii. Musa alisema Yeye angekuwa ni Nabii; Naye alikuwa na Nguzo ya Moto, na akafanya ishara na maajabu. Na nabii yuyo huyo akasema, ya kwamba, "Kila aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

266 Na hapa Yeye aliahidi jambo lile lile katika kule kutoka katika siku za mwisho, wala hawezi kulibadili. Na kwa thibitisho la kisayansi, kwa ushuhuda wa Roho, kwa kazi za Roho, tunaona jambo hilo siku hizi, ile Nguzo kuu ya Moto ikitenda kazi miongoni mwetu; na ishara na maajabu ya kufufuka kwa Yesu Kristo, akiwaita watu kutoka katika umadhehebu, waingie katika Uwepo wa Yesu Kristo, wakaishi, waende kwenye Nchi fulani. Hakuna kosa, enyi marafiki. Si yale ninayosema mimi; mimi ni ndugu yenu tu. Lakini, ni yale Mungu anayowathibitishia, ndiyo yanayolifanya Kweli. Nguzo ile ile ya Moto aliyoitumia kwenye kule kwingine kuwili, Yeye ameileta miongoni mwenu leo, na kuithibitisha kisayansi. Kama mjuavyo, gazeti la *Life* lililiandika mwezi uliopita, huko juu. Ambapo . . .

267 Ni wangapi waliokuwa hapa na wakanisikia nikisimulia habari hiyo, kile kilichotukia, kabla halijatukia? Nafikiri, karibu kila mtu humu kanisani.

268 Hiyo hapo. Hawajui ina maana gani; wanasayansi wanajaribu kuichunguza. Mtu yeyote aliye na picha Yake, walipiga simu, "Wingu, maili ishirini na sita kwenda juu, katika umbo la piramidi." Malaika saba wakiwakilishwa mle, walirudisha na kuwaletea Neno la Mungu, chini ya uvuvio. Inawaambia majira haya mnayoyaendea na mnayoishi. Watu wa kiroho watalishika hilo sasa hivi, unaona, na kulipata. Ni kutoka. Tutaondoka, moja ya siku hizi. Mungu na ashukuriwe. Kumbukeni.

Nami nitafunga, kidogo tu. Nina dakika kumi.

269 Angalieni ile Nguzo ya Moto iliyowaita watoke, ikawaongoza kwenye nchi ya ahadi, chini ya upako wa nabii. Nguzo ya Moto ambayo wangeweza kuiangalia, iliwaongoza kwenye nchi ya ahadi, chini ya nabii aliyetiwa mafuta. Nao daima walimkataa. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika.

270 Sasa, ninajua hatuna budi kufanya ibada ya ubatizo. Nina kama kurasa sita zaidi hapa, nadhani. Lakini nitaacha sasa, katika dakika moja.

271 Angalia jambo hili. Tuko katika kuitwa tutoke. "'Tokeni Babeli, enyi watu Wangu,' ilisema sauti ya malaika." Kutoka

kwenye nini? Machafuko. Je! Methodisti ndiyo sahihi, ama ni Baptisti, ama Katoliki? "Tokeni kwake." Mungu yuko sahihi. Unajuaje? "Acha neno la kila mtu liwe ni uongo, na Langu Kweli. Tokeni kwake." Unajua nini? Nguzo ile ile ya Moto, Roho yeye yule wa upako, akiongoza kwenda kwenye Nchi ya ahadi.

272 Angalieni, aliwaongoza, akawatoa, akawaongoza hadi kwenye nchi ya ahadi; Israeli, taifa.

273 Na Mungu yeye yule, Nguzo ile ile ya Moto! Hiyo huninii tu . . . "Wao wanasema ya kwamba ninii . . . ya kwamba hiyo kamera . . . " Mnaposoma George J. Lacy; sio mimi, sasa. Mnasoma ambapo George J. Lacy alipoichunguza picha hiyo. Mkubwa wa F.B.I., wa alama za vidole na hati, hilo hapo tamshi lake. "Mtu fulani anasema, 'Lenzi iliyoingizwa mwanga maradufu.'" Makumi elfu ya watu wameiangalia, kwa macho yao wenyewe. Tulisimama hapa na kuiangalia. Mmeiangalia. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sivyo. "Walisema, 'Ilikuwa ni mazingaombwe.'" Bw. Lacy alisema nini? "Jicho la kimitambo la kamera hii haliwezi kupiga picha saikolojia." A-ha. Hayakuwa ni mazingaombwe. Ipo, Nguzo ile ile ya Moto.

Kisha wanasema, "Loo, vema, hiyo ilikuwa ni udanganyifu wa kimawazo."

Sasa, kamera mbalimbali, zote, kwa mamia ya maili kuuzunguka Tucson!

274 Miezi sita kabla halijatukia, tuliwaambia, kwa Roho Mtakatifu, nitakuwa nikienda huko kupata habari. Kwa sababu, Maandiko ya piramidi hiyo yako upande wa nje, kama yule ndugu alivyokuwa ameota ndoto, nami nikawafasiria hayo. Hiyo ndiyo fasiri nzima. Sasa, siri zote za kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, zilikuwa tayari zimeelezwa. Sasa ni kuokota vipande vilivyoachwa vya hayo, ambavyo vilikuwa vimefichwa katika ile Mihuri Saba, sio kwenye yale makanisa saba. Mihuri saba inazifunua zile siri. Na kisha akakifunua kitu hiki, kwenye kilele, na akakuta Mwamba mle ndani, mweupe, bali kamwe haujaandikwa chochote juu yake. Ilikuwa ni siri.

275 Kaenda Tucson; kalitabiri kabla halijatukia. Kasimama kaskazini mwa Tucson, mashahidi wamesimama hapa nalo, wakati mlipuko ulipotokea, ambao uliitikisa milima chini, karibu kuiangusha. Na wakati ule ule, duara ya nuru ikining'inia huko hewani, wakati sayansi ilipozipiga zile picha sasa. "Maili ishirini na sita kwenda juu," karibu mara tano umbali ambao ukungu ama chochote kile ungeweza kuwa. Wala hata hawawezi kujua ni kitu gani kilichoisababisha.

276 "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Njia ya Utukufuni hakika mtaipata, kama umeteuliwa. Mbegu hiyo ikianguka juu ya nchi kavu, juu ya miamba, kamwe haitafanya kitu; mioyo migumu,

ya mawe ambayo inataka kuwa isiyojali. Bali endapo itaanguka kwenye ardhi laini nyororo ya imani, itamzaa Mkristo, anayezaa matunda ya Roho.

277 Angalia jinsi ambavyo Mungu alifanya jambo hilo. Sasa Yeye ana Nguzo ile ile ya Moto. Hiyo imethibitishwa.

Mtu fulani alisema, “Kwa nini usiende ukawaambie hao wanasayansi kuhusu jambo Hilo?”

278 Unafikiri wataamini Hilo? “Msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe.” Yesu alisema tusizitupe. Sina miongozo ya kufanya hivyo, ingawa ninaishi mumo humo kwenye jiji ambamo walikuwa wakiulizia hilo. Nilidhani ningeshuka niende kule. Roho Mtakatifu akasema, “Usiende. Si kwa ajili yao. Rudi na ukaambie maskani.” Vema.

279 “Na itatukia. Kama yale wanayosema yakitimia, basi, kumbukeni, Mimi nimenena,” asema Bwana, “unaona, kabla halijatukia.” Hilo hapo linatukia. Isikilizeni Biblia, Sauti ya Mungu ikiwaita katika siku hii.

280 Sasa ninawatakeni muone. Nguzo ii hii ya Moto inawaongoza watu tena kwenye Nchi ya ahadi, ule Utawala wa Miaka Elfu. Ambapo, tuliona, chini ya uvuvio wa Muhuri huu wa Sita, (halijafundishwa hapo kabla), jinsi ambavyo dunia haina budi kusafishwa kwa ajili ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Ile Nguzo ya Moto inawaongoza kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu.

281 Na hebu angalieni ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza Israeli kutoka kwenye utumwa, katika kule kutoka; ile Nguzo ya Moto, chini ya uongozi wa Mungu . . . Mungu alikuwa ni ule Moto, na ile Nguzo ya Moto ilimtia mafuta tu yule nabii. Ile Nguzo ya Moto ilikuwa isimame kama ushahidi wa Mbinguni kwamba Musa alikuwa ameitwa atoke.

282 Kumbukeni Dathani, hao, walisema, “Vema, inatupasa kuanzisha dhehebu. Musa, unajichukulia mengi sana. Unajaribu kusema wewe ndiwe mtu pekee kati yetu aliye mtakatifu. Kusanyiko lote la Bwana ni takatifu. Unawezaje kujitwika jambo hili?”

283 Ndipo Musa akaanguka kifudifudi akaanza kulia. Mungu akasema, “Jitenge naye. Nitaifunua tu nchi na kummeza.” Mfano. Inawezekanaje . . . Musa akawaambia ya kwamba yeye alikuwa akiwaambia yale Mungu aliyokuwa amesema, Mungu akiyathibitisha kwamba ni Kweli.

284 Hata Miriamu, yule nabii mke mwenyewe, na Haruni, walimcheka Musa, kwa ajili ya kumwoa yule msichana wa Kushi, wakimdhihaki. Naye Mungu akakasirika; kuongea dhidi ya mtumishi Wake. Alifanya nini? Aliwaita watoke nje waende kwenye mlango wa maskani. Naye Miriamu, hata hivyo, alikuwa ni nabii mke. Bali Musa alikuwa ni zaidi ya nabii, zaidi ya nabii.

Akasema, "Hivi hammwogopi Mungu? Akiweko nabii kati yenu, Mimi Bwana nitasema naye katika maono, na kujitambulisha kwake kwa ndoto, bali," kasema, "sivyo Musa." Kasema. "Hivi hammwogopi Mungu?" Na yeye—na yeye alikuwa amekufa nusu kwa ukoma, dakika hiyo. Mnajua jambo hilo.

285 Hivi Yeye hakusema, "Yohana Mbatizaji. Je! mlitoka kwenda kumwona nabii? Naam, zaidi ya nabii"? Kwa nini? Ni kwa nini yeye alikuwa ni zaidi ya nabii? Yeye alikuwa ni mjumbe wa Agano, lile sanduku lililoshikamanisha vipindi hivyo viwili pamoja.

286 Na leo hii, ninii. . .kile tulicho nacho miongoni mwetu, huyu Roho Mtakatifu mkuu, ni zaidi ya nabii. Ni Mungu aliyedhihirishwa miongoni mwetu, pamoja na Neno Lake kuthibitisha jambo hilo. Anafanya zaidi ya nabii, mara elfu zaidi ya yale manabii wafanyayo.

287 Eliya, mmoja wa manabii walio wakuu sana wa wakati, alifanya tu mambo manne ya kimbinguni, katika maisha yake yote ya miaka themanini na kitu. Naye Elisha, akiwa na sehemu maradufu, alifanya minane.

288 Nasi tunaona maelfu mara maelfu, kwa macho yetu wenyewe, tunamwangalia Malaika wa Bwana, katika Nguzo ya Moto. Uchunguzi wa kisayansi, ukilipeleka ulimwenguni, tukijua ya kwamba watahukumiwa kwa Hilo. Yule Mwana-Kondoo alifanya nini, yule Malaika wa Bwana, ambaye alikuwa ni Kristo? Mnaliamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

289 Yohana Mtakatifu 6. Wote walikuwa wakinywa maji haya, huku wakiwa na wakati mzuri sana na kushangilia. Yeye akasema, "Mimi Ndimi Chakula cha Uzima kitokacho Mbinguni kwa Mungu. Mimi Ndiye ule Mwamba uliokuwa nyikani."

290 Wao wakasema, "Sasa tunajua Wewe una kichaa. Wewe ni—wewe ni mwenda wazimu. Wewe, Wewe una pepo juu Yako. Wewe ni Mtu mwenye kichaa, mwenye pepo." Unajua, watu wakiingiwa na pepo, wakati mwingine wanachangamka sana, wanakuwa wa kidini. Walisema, "Wewe ni—Wewe ni pepo. Una pepo juu yako. Wewe ni Msamaria, na una pepo juu Yako." Kasema, "Na hapa, Wewe hata hujapata zaidi ya umri wa miaka hamsini, na unasema ati Wewe 'ulimwona Ibrahimu'?"

291 Naweza kumwona akirudi nyuma hatua chache. Kasema, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Huo ulikuwa ni Moto unaowaka, ile Nguzo ya Moto kichakani.

292 Wakati alipokufa, na akafufuka siku ya tatu, na Sauli akakutana na Yeye njiani akienda zake, Yeye alikuwa amerudi akawa hiyo Nguzo ya Moto. Kasema, "Ninatoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu."

293 Wakati Petro alipokuwa gerezani, hiyo Nguzo ya Moto iliingia, ikaifungua milango na kumpeleka nje. Hiyo ni kweli.

Hiyo Nguzo ya Moto iliwaelekeza wapi?

294 Sasa, kumbukeni, Musa hakuwa hiyo Nguzo ya Moto. Yeye alikuwa ni kiongozi aliyetiwa mafuta, chini ya hiyo Nguzo ya Moto, na hiyo Nguzo ya Moto iliuthibitisha tu Ujumbe wake kwa ishara na maajabu.

295 Na hiyo Nguzo ya Moto iliwaongoza kwenye nchi ambayo Mungu aliwaahidi, ambako Yeye, Mwenyewe, angefanyika mwili miongoni mwao, siku moja. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Walifanya nini? Walinung'unika na kufadhaika, na chochote kile, kuonyesha ilikuwa chini ya damu ya mwana-kondoo wa kawaida.

296 Lakini wakati huu (utukufu kwa Mungu), Nguzo tunayoiona miongoni mwetu, hiyo Nguzo ya Moto itatuongoza kwenda kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, ambako Yeye atawarudia watu Wake kwenye ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu baada ya huku kutoka, ambako tutaishi Milele pamoja na Yeye. Yeye daima ana Neno la Baba, daima anathibitisha kwamba ni kweli.

297 Tuko kwenye kutoka. Na tukiondoka, na kuzizima kanda kwa muda kidogo. Loo, enyi rafiki zangu, ndugu zangu, mlioko na wale mtakaosikia kanda, hebu mimi . . . kama ndugu yenu na raia wa Ufalme wa Mungu. Tokeni, katika kutoka huku, kwa maana wote watakaoachwa nyuma watatiwa alama ya mnyama. Tokeni Babeli. Tokeni kwenye mchafuko huu. Tokeni kwenye mifumo hii, na mkamtumikie Mungu aliye hai. Hebu . . .

298 Malaika huyu mkuu wa Agano! "Yesu Kristo, akiwa yuna namna ya Mungu, hakuona ni kitu cha kushikamana nacho, bali akawa sawa na Mungu." Sasa Yeye ni Nguzo ya Moto, katika umbo lile lile alilokuwa nalo huko nyuma, akikuleta kule kutoka kwa kwanza, akikuleta kule kutoka kwa pili, na Huyu hapa akiwa na huku kutoka kwa tatu.

299 Kule kutoka kwa kwanza, Yeye alifanya nini? Aliwatoa katika nchi ya kawaida, akawapeleka kwenye nchi ya kawaida.

300 Kutoka kwa pili, Yeye aliwatoa kutoka katika hali ya kiroho, akawaingiza katika ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu.

301 Sasa Yeye anawaleta kutoka kwenye ubatizo wa kiroho wa Roho Mtakatifu, anawarudisha moja kwa moja katika Nchi ya Milele ya ule Utawala wa Miaka Elfu na Mambo makuu ya Baadaye. Nguzo ile ile ya Moto, kwa mfumo ule ule uliotiwa mafuta, Mungu yeye yule akifanya mambo yale yale! Na Neno lile lile, lililotangaza kule kwa kwanza, lilikutangaza kule kwa pili. Neno lile lile, lililokutangaza kule kwa pili, limekutangaza kwa tatu, na hapa tunakuona miongoni mwetu.

302 Tokeni. Loo! Tokeni kwenye machafuko haya. Njoni kwa Mungu aliye hai. Njoni kwenye Neno. "Naye Neno alifanyika

mwili, akakaa miongoni mwetu." Na sasa Yeye yumo mwilini mwetu, akiishi miongoni mwetu. Tokeni mje mkamtumikie Mungu aliye hai.

303 Wakati tukiinamisha vichwa vyetu. [Ndugu fulani ananena kwa lugha. Ndugu mwingine anatafsiri—Mh.]

304 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Kutoka katika vilindi vya nafsi yako, kutoka kwenye vilindi vya yote yaliyo ndani yako, je! uko tayari kukumbuka kuninii . . . Je! uko tayari kuacha mambo yote ya ulimwengu, na umwishie Mungu? Sasa, kama humaanishi jambo hili, usilifanye. Bali endapo unalimaanisha, kwa moyo wako wote, ya kwamba sasa umeshawishika. Kama Yesu alivyosema, mwishoni mwa huduma Yake, "Je! sasa mnaamini?" Je! umeshawishika ya kwamba mambo haya ni kweli, yamethibitishwa na Mungu, na kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho, na kweli unataka kumjia Kristo sasa? Njoo katika kutoka huku, kwa kuitwa kutoka kwenye kutojali, umadhehebu, mawazo na mambo ya ulimwengu. Na unataka kujitolea Kwake kwa moyo wako wote na utoke katika kutoka, kwa ajili ya ile Nchi ya ahadi iliyobarikiwa, je! utainua mikono yako wakati tukiomba? Je! una hakika kweli ya kwamba unataka kutoka, kila mtu?

305 Baba wa Mbinguni, wale walioinua mikono yao juu, jalia watoke sasa, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu, juu ya ahadi ya Neno, jalia Roho Mtakatifu aingie mioyoni mwao. Kutoka kwenye kusanyiko letu, kulikuwako na karibu mikono ishirini, nadhani, Baba, ambayo imeridhika na wanajua ya kwamba ni—ya kwamba ni kweli, nao wanataka kutoka. Kama kulikuwako na . . .

306 Katika zile siku za kuja kwa Israeli, kutoka katika watu milioni mbili na nusu, ni wawili tu waliofaulu kuingia nchini.

307 Katika siku za Yesu Kristo, kulikuwa na karibu mia moja na ishirini waliofaulu.

308 Na sasa, katika siku za mwisho wa ulimwengu, Wewe ulisema, "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, na lakini ni wachache watakaoiona. Bali njia ni pana iendayo upotevuni, na wengi wataingia humo." Maneno hayo hayawezi kushindwa. Ni Yako.

309 Sasa ninawaombea, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utaninii, saa hii, kwa Roho Wako Mtakatifu, utaitahiri mioyo yao. Ondoa mambo yote ya ulimwengu. Yatahiri maskio yao, kwa kuwa wanaweza kusikia Sauti ya Mungu dhahiri, ikiita, kupitia Neno Lake na kupitia Nuru ya siku hizi. Na uwajalie, Bwana, ya kwamba macho yao yatafunguliwa, wapate kuona utukufu wa Mungu katika saa hii ya mwisho ya kumalizia. Wewe ulisema, "Wote alionipa Baba watakuja, Nami nitawafufua katika siku ya mwisho."

310 Bwana, labda kuna wengi hapa ambao bado hawaelewi. Ninaomba ya kwamba Wewe utawashughulikia, na utawajalia kupata nafasi nyingine, Bwana, kusudi wapate kufahamu, kukusikia Wewe ukinena kupitia Neno Lako, ukijithibitisha Mwenyewe, na halafu unene nasi katika sauti ya kimbinguni, na halafu kwa ufasiri; kuona kazi Zako kuu zikilithibitisha kwamba ni kweli, kulingana na Biblia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utatusamehe dhambi zetu, sasa, wakati nikijilaza kwenye Neno hili.

311 Mungu, ninawazia ya kwamba, juma moja tu lililopita, ni—nilijilaza juu ya mtu aliyekufa hapa sakafuni. Nilimwona Roho Mtakatifu mkuu akimrudishia uhai wake. Macho yake yaligeuka tena nyuma ya kichwa chake, akilala, amekufa. Maneno madogo tu, machache, ya kuliitia Jina Lako, nilimwona akifufuka. Huyu hapa leo, yu hai, bado. Bwana, Wewe ni Mungu yeye yule, ambaye, wakati Paulo alipojilaza juu ya yule mvulana, akimsikiliza akihubiri kwa muda mrefu, yule mtu aliyeanguka kutoka dirishani. Wewe ni Mungu yeye yule anayeweza kuurudisha uhai. Tunakushukuru, Baba. Jalia . . . Asiyeamini huenda asiamini. Lakini sisi tunaamini, Bwana. Wewe umejithibitisha Mwenyewe kwetu.

312 Sasa jalia tafakuri ya moyo wangu, na mawazo ya roho yangu, nguvu zangu na kadhalika, ziyeyushwe katika Neno hili. Pia jalia Neno pamoja na mimi, pamoja, Bwana, pamoja na watu hawa, tutembee kiaskari kuelekea kwenye Ufalme wa Mungu. Tujalie, Bwana. Tusamehe dhambi zetu. Yaponye magonjwa yetu, na utufanye raia wa Ufalme Wako.

313 Na sasa, wakati hawa wakija, Bwana, na kidimbwi kinafunguliwa, maji yako tayari, na ubatizo utaanza katika dakika chache, tunakumbuka wakati Injili ii hii ilipohubiriwa, Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa."

314 Hizi hapa leso zimewekwa hapa, Bwana, ninazozibariki katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wa wagonjwa. Halafu wakati . . .

315 Ibada zetu ni ndefu, zimerefuka, kwa kuwa saa zimeenda sana. Inatupasa kupanda Neno wakati kukiwako na shamba la kulipandia, kwa kuwa majira ya baridi kali yanakuja. Tunayaona. Majani yanapukutika, nasi tunajua ya kwamba majira ya baridi kali yamekaribia. Hatuna budi kukwaruza udongo na kuizika Mbegu. Kwa hiyo, ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Wewe utanena na kila moyo.

316 Na Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa." Na, Bwana, kama kuna wengi hapa sasa ambao wameamini, wala hawajabatizwa bado katika Jina la Mwanao mpendwa, Yesu, jalia waje asubuhi ya leo, kwa utamu na unyenyekevu, na huku wakiitubia dhambi yao, na wakiyafia mambo ya ulimwengu; wapate kuzikwa, kulichukua Jina la Yesu Kristo; kuishi kitaua,

tangu sasa na kuendelea, kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Tunawakabidhi Kwako sasa, Bwana, kwa kusudi hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

317 Sasa tunairudisha ibada kwa Ndugu Neville, na lolote analotaka kusema, wakati tukijiandaa kwa ajili ya ibada ya ubatizo.

318 Na usiku wa leo, kwenye saa moja na nusu, Bwana akipenda, ninataka kuurekodi Ujumbe huu mwingine. Mungu awabariki hadi wakati huo.

*KUTOKA KWA TATU* SWA63-0630M
(The Third Exodus)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 30 Juni, 1963, kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org